# Nipashe

Jumatatu Aprili 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580210

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

dian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





Nipashe Spotika

CAVANI NI SASA EPL AU KAMWE? UK. 12 & 13

ISIKUPITE

KLABU 4 ANAZOWEZA KUTUA AUBAMEYANG

UKURASA 11

## Wenyeviti mbaroni madai kugeuza karantini biashara

UKURASA 4

# Wanaoingia Muhimbili sasa kupuliziwa dawa

• **Mbunge** Chadema apendekeza mambo saba kukabiliana na ugonjwa... *Endelea ukurasa wa 2*



### BAA LA CORONA

**Upokwenda kununua bidhaa dukani (supermarkets), kaa umbali wa mita moja. Kama kuna ulazima safisha mikono ya tolori au kikapu cha kubebea bidhaa kwa vitakasa mikono kabla ya kufanya ununuzi. Unapofika nyumbani, safisha mikono pia baada ya kushusha bidhaa. Hakuna kisa kilichothibitishwa mpaka sasa cha kupata maambukizi ya Covid-19 kupitia chakula au vifungashio. WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabauni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

TOLEO MAALUMU

## Hakika Dk. Reginald Mengi ameacha alama

UKURASA 3




Wananchi wakipita kwenye mashine maalum yenye dawa ya kunyunyiza, iliyowekwa kwenye geti la kuingilia Hospitali ya Taifa Muhimbili Dar es Salaam, kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19. **PICHA: JUMANNE JUMA**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store


## Wagonjwa 23 wapya wa corona wagundulika Z'bar

UKURASA 17


**MICHEZO** LUSAJO AISHUSHA PRESHA NAMUNGO UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mambo 7 Mbunge Chadema

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Upendo Peneza, ameishauri serikali mambo saba, ikiwamo kupunguza misongamano na kuwasilisha bungeni bajeti ya dharura ya kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana, Peneza ambaye pia ni Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alisema licha ya nchi kuendelea kuchukua jitihada za kukabiliana na ugonjwa huo bado kuna misongamano.

**MISONGAMANO**

Alisema bado hakuna jitihada za kutosha kukabiliana na misongamano kwenye vyombo vya usafiri, masokoni na ofisini, huku akishauri watu wafanyie kazi majumbani.

Alisema kuna nchi zinajifungia ndani watu hawatoki lengo ni kupunguza maambukizi kwa kuwa wakiambukizwa wengi madaktari waliopo watashindwa kutoa huduma. Aliongeza: "Kuna misongamano maeneo ya masoko bado watu wanajazana bila kuvaa barakoa wala kupeana umbali. Watu wanaoingia sokoni bado wanagongana gongana na kusogeleana sana, na kujiweka katika hatari kupata ugonjwa."

Alibainisha kuwa kwenye magulio na minada, serikali inapaswa kuweka usimamizi mkubwa kwa kuhakikisha watu wakae umbali wa mita moja na si kama ilivyo hivi sasa.

**MAOFISINI**

Kuhusu maofisini, Peneza alishauri serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kuweka utaratibu wa wafanyakazi kuingia wachache wachache.

"Si lazima watu wote waende kazini saa moja na kurudi saa 10, serikali katika Wizara na Ofisi mbalimbali ina vitengo, utakuta kitengo kimoja kina watu 20 au 30 ni kupanga tu wengine waingie saa moja asubuhi hadi saa sita mchana na wengine saa sita hadi jioni ili kuondoa msongamano kwenye usafiri na ofisini," alisema.

Pia alisema serikali ishauri sekta binafsi watu wafanye kazi kwa kuachiana ili kuepuka msongamano na watu wafanyie kazi nyumbani kadri inavyowezekana.

**NYUMBA ZA IBADA**

Aliishauri serikali kukaa na viongozi wa dini kusaidia watu kusali wakiwa nyumbani kupitia Televisheni ya Taifa na kupunguza idadi ya watu wanaoingia kanisani.

"Kuna Askofu kule Ngara ametoa waraka waumini wake hawatakwenda kanisani kwa siku 40, lakini serikali inatuonyesha umuhimu wa kusali, bado inaweza kuwasaidia watu kusali wakiwa nyumbani na kupunguza idadi ya watu wanaoingia kanisani, watumie chombo cha Taifa, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili." Kuhusu utaratibu wa kutoa sadaka na zaka, Peneza alishauri makanisa yaweke utaratibu wa watu kutoa fedha kupitia benki au kwa njia ya mtandao ili kuepuka kushika fedha.

**KUKAA KWA UMBALI**

Alisema pamoja na kumuomba Mungu ni vyema Watanzania wakazingatia kukaa kwa umbali ulioshauriwa na wataalamu.

**BAJETI YA DHARURA**

Alisema serikali inatakiwa ijiandae na kupeleka bungeni ili lipitishwe fungu maalum la fedha za dharura kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi pale nchi itakapoingia kwenye 'lockdown'. "Lazima tuwafikirie watu ambao kazi zao zinategemea wengine ili waweze kula, tusimamie suala la kukaa kwa umbali ili Mungu aone tupo makini," alisema.

Aidha, aliitaka serikali iseme ina vifaa kiasi gani vya kukabiliana na corona.

**BEI YA BARAKOA**

Alisema bado bei ya barakoa ni tatizo kwa mwananchi wa hali ya chini kwa kuwa zinatakiwa kuvaliwa na zimeshauriwa na wataalamu bei yake ya chini ni Sh.3,000 na inatakiwa kuvaliwa kwa saa.

**KUFUNGA MIPAKA NA BAA**

Alisema ugonjwa huo ni vita, hivyo ni muhimu kufunga maeneo ambayo yataonekana yanachochea maambukizi.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa (katikati), Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kampuni na Majina ya Biashara (BRELA), Meinrad Rweyemamu (kushoto), wakisikiliza maelezo kutoka kwa Kamishna wa Magereza, Uwesu Ngarama, aliyemwakilisha Kamishna Jenerali wa Magereza, wakati wa makabidhiano ya jengo la ofisi jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wanaoingia Muhimbili lazima kupuliziwa dawa

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imeanza kuchukua hatua dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona, baada ya jana kufunga mashine mbili za kutakasa mwili na mvuke wenye dawa.

Mashine hizo zilizowekwa kwenye geti la kuingilia katika hospitali hiyo, zitawezesha wagonjwa na wananchi wanaofika kupata huduma ya kunyunyuziwa dawa kabla ya kuingia katika viwanja vya hospitali hiyo.

Lengo kuu la kufungwa kwa mashine hizo maalumu ni kuhakikisha hospitali hiyo na wafanyakazi wake wanakuwa salama wakati wote, ili iweze kuhudumia Watanzania kama Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alivyoelekeza.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, mashine hizo zimetolewa kama msaada na mmoja wa wafanyabiashara wakubwa nchini ili kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili unamshukuru kwa msaada huo. Mahitaji bado ni mengi, tunaomba wasamaria wema kusaidia kupata mashine kama hizo 12 ili ziwekwe maeneo mbalimbali ya Muhimbili," alisema Aligaesha.

Mwishoni mwa wiki, MNH iliwataka ndugu wote wanaokwenda kuona wagonjwa na wadau wengine watakaofika katika hospitali hiyo kuhakikisha wanavaa barakoa (mask) kwa lengo la kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo hatari. Vilevile, Waziri Ummy alitoa tahadhari kwa wananchi wenye dalili za ugonjwa huo kutokwenda kupima MNH, badala yake waende Hospitali ya Rufani ya Amana.

Waziri Ummy alieleza kuwa MNH ndiyo hospitali kubwa ya rufani ya Taifa ambayo inahudumia Tanzania Bara na Zanzibar, hivyo inahitaji kuwekwa katika uangalizi maalum.

Alisema MNH ndiyo inayotoa matibabu ya kibingwa na bobezi, hivyo serikali imeamua kuiteua Hospitali ya Rufani ya Amana kuchukua wagonjwa wa corona.

"Tumeamua kupokea wagonjwa wa corona katika hospitali ya Amana kwa lengo la kui-protect (kuikinga) hospitali ya Muhimbili," alisema Waziri Ummy. Waziri Ummy alisema MNH ndiyo inayofanya upasuaji wa mifupa na mishipa ya fahamu, magonjwa ya moyo, matibabu ya kibingwa ya figo, kupandikiza vifaa vya kusikia, na magonjwa makubwa. Alisema kama ikiachwa, Watanzania waendelee kwenda katika hospitali hiyo kiholela, maana yake hakutakuwa na sehemu nyingine ya kukimbilia kupata matibabu.

Hadi kufikia jana, idadi ya watu walioambukizwa virusi vya corona Tanzania walikuwa 170, baada ya ongezeko la wagonjwa wapya 23 Zanzibar.


**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.109/2014**

**ELIYA AMBAKISYE JONGO::::::::::::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**FELIX JAMES MSUKWE:::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA 1**

**KALOLO BERNARD KAMBI::::::::::::::::::::::::MDAIWA 2**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA:KALOLO BERNARD KAMBI**

Fahamu kwamba Eliya Ambakisye Jongo amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 21/04/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.

**Kumbuka:**Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 23/03/2020.

T. Munzerere
Mwenyekiti

23/03/2020



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA. 289/2019**

**CLEZENSIA AVITH/YUSTINA AVITH………………WADAI/WASHINDI**

**DHIDI YA**

**GASTON GASPARY……………….WADAIWA/WASHINDWA**

**KWA: GASTON GASPARY – POPOTE PALE MLIPO**

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na. 289/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 21.04.2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi. Hivyo unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 23.03.2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA



**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**STEPHEN MUSSA STEPHEN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 496 BXN SANLG,** CHASIS NAMBA **LBRSPJB56J9012424,** ENGINE NAMBA **SL 18914962** KUTOKA KAMPUNI YA WU 2HOU INVESTMENT. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU APIGE SIMU NAMBA **0786-888888 / 0765-967390.**
**RB NAMBA SHY/TR/RB/ 426/ 2020.**



**ANATAFUTWA**



**JOSEPH JOHN MUNISHI** miaka 24, mzaliwa wa Kitandu Kibosho Mango ANATUHUMIWA KUTOROKA NA FEDHA ZA MWAJIRI WAKE ZAWADI ITATOLEWA KWA TAARIFA ZA KUKAMATWA KWAKE.

Piga namba 0754279966 au 0784475378.Taarifa ya Police MDP/RB/220/2020.

TOLEO MAALUM



Dk. Reginald Abraham Mengi

"Fursa zina aibu, zinasubiri uzikimbilie"

# Dk. Reginald Mengi hakika ameacha alama

**Na Romana Mallya**

UKIZUNGUMZIA mapinduzi ya viwanda nchini, Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ni miongoni mwa Watanzania wachache walioanzisha viwanda mbalimbali vinavyozalisha bidhaa za masoko ya ndani na nje pamoja na kutoa ajira kwa wingi.

Dk. Mengi, maono yake yanaendelea kuishi na Watanzania wanaendelea kufurahia maisha yake ambayo yameacha alama kubwa kwenye taifa kupitia ubunifu wake katika uwekezaji ambao umewezesha utoaji ajira, na kampuni zake kuchachangia Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Katika kuhakikisha anaacha alama isiyofutika, alipenda kueleza kwa uwazi historia ya maisha yake alikotoka, alikopita, mpaka mafanikio.

**SAFARI YA MAFANIKIO**

Mafanikio yake yanatokana na uthubutu aliouonyesha kwa vitendo.

Baada ya kumaliza masomo yake nchini Uingereza mwaka 1971, aliajiriwa kwenye kampuni ya Coopers and Lybrand Tanzania, ambayo kwa sasa inajulikana kama Price Waterhouse Coopers.

Baada ya kufanya kazi kwa muda, alijiengua na kuanzisha kampuni ya IPP katika miaka ya 1980.

Kampuni hiyo anzilishi ilijishughulisha na utengenezaji wa bidhaa mbali mbali muhimu kulingana na mahitaji ya soko ya wakati huo. Dk. Mengi, alianza kama mjasiriamali mdogo aliyethubutu kujaribu kila biashara na ilipofanikiwa alikuwa akiongeza nyingine.

Alianza kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo kalamu za wino, viatu, dawa ya kuziba nyufa, rangi za kung'arisha viatu, vitakasa sakafu, chaki, mishumaa, dawa za kuulia wadudu na dawa za chooni. Vyote hivyo alivitengeneza kwa kutumia teknolojia nyepesi, kama wafanyavyo wajasiriamali wadogo wa sasa.

Bidhaa hizo zilizomtengenezea jina kubwa kutokana na umuhimu wake, ni pamoja na mafuta ya mgando, kalamu za wino na ilifika hatua akajikita kwenye uzalishaji wa vyombo vya plastiki vikiwamo vikombe, sahani na bakuli.

Alitengeneza pia, chupa za chai, magodoro, mito, vifaa vya umeme, karatasi maalumu za chooni (toilet paper) na dawa ya meno.

Hakuishia hapo, alitengeneza mashine za kutengeneza tofali, samani za ndani za mbao na chuma, na vifaa vya ujenzi.

Uthubutu wake ulimuwezesha kubuni michezo ya kubahatisha (Bingo), pombe kali kama Whiskey, Brandy, na Gin.

Alikuwa pia msambazaji wa bia aina ya Carlsberg na alitengeneza sabuni za kuogea maarufu kama Revola, Amanda, Evita na Protex.

Sabuni za unga zilizotengenezwa na viwanda vyake ni Tessa na Dynamo na sabuni za mche maarufu kama Komesha.

Dk. Mengi pia alianzisha vyombo vya habari vya ITV/Radio One, mwaka 1994 na magazeti ya The Guardian na Nipashe, mwaka 1995.

Baadaye vyombo hivyo vya habari viliongezeka kikaanzishwa kituo cha televisheni cha Afrika Mashariki na redio (EATV/EAR) na Capital Televisheni na radio.

Magazeti pia yaliongezeka na kuanzishwa ya wiki ya Kiswahili na Kiingereza kama Nipashe Jumapili, Sunday Observer, Kulikoni, ThisDay na Lete Raha, yote yakiwa chini ya kampuni ya magazeti ya The Guardian Limited maarufu kama The Home of Great News Papers.

IPP pia inajumuisha viwanda vinavyozalisha vinywaji baridi, wazalishaji wa maji ya Kilimanjaro, soda zinazozalishwa na kampuni ya Bonite Bottlers, wazalishaji wa soda tofauti chini ya kivuli cha Coca-Cola.

Dk. Mengi amekuwa nuru na mwanga kwa maisha ya Watanzania hususan vijana ni alama ya kihistoria Tanzania kwa kuacha maelfu ya ajira katika sekta ya viwanda, habari na biashara.

Ukarimu, upendo, uthubutu na uzalendo wake, alijishusha ili kuonyesha kuwa binadamu wote ni sawa bila kujali tajiri au maskini.



Dk. Reginald Mengi akiangalia bidhaa katika mabanda ya wajasiriamali kwenye Maonyesho ya Kimataifa viwanja vya Mwalimu J K Nyerere jijini Dar es Salaam.





Bidhaa ya 'toilet paper' na sahani ni moja kati ya zinazotengenezwa na viwanda vya Dk. Reginald Mengi.

*Itaendelea kesho*

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**MAMLAKA** ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa Ripoti ya Utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini kwa mwaka 2018/19, ikihusisha Mamlaka za maji za Mikoa na Miradi ya Kitaifa 34 na Mamlaka za Wilaya na Miji Midogo 83.

Ripoti hiyo iliyotolewa Machi 2020, inabainisha kuwa utoaji huduma umeimarika katika kiwango cha maji yaliyozalishwa; idadi ya watu wanaopata maji; ubora wa maji; wateja wa maji na wateja wa mtandao wa uondoaji majitaka; uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja; na makusanyo na ufanisi cha ukusanyaji maduhuli.

Vilevile Ripoti hii ya utendaji imebainisha changamoto zinazozikabili mamlaka za maji ikiwemo kiwango kikubwa cha upotevu wa maji; kiwango kidogo cha maji yanayozalishwa ukilinganisha na mahitaji; na utoaji huduma ya uondoshaji majitaka usiokidhi mahitaji. Aidha, Ripoti hiyo imeainisha mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo na kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira zinazotolewa na mamlaka za maji nchini.

Katika Ripoti ya mwaka 2018/19, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zilizoibuka Kinara katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira ni MOSHI kwa upande wa Mamlaka za Maji za Mikoa; **MAKAMBAKO** kwa upande wa Mamlaka za Maji za Wilaya na Miji midogo; na **KASHWASA** ambayo imeibuka kinara kwa upande wa Miradi ya Kitaifa.

Mamlaka zilizoshika nafasi ya Pili kwa ubora katika utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ni IRINGA kwa upande wa Mamlaka za Maji za Mikoa; MIKUMI kwa upande wa Mamlaka za Maji za Wilaya na Miji midogo; na Masasi-Nachingwea **(MANAWASA)** kwa upande wa miradi ya Kitaifa.

Mamlaka zilizoshika nafasi ya Tatu kwa ubora katika utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ni **MWANZA** kwa upande wa Mamlaka za Maji za Mikoa; **BIHARAMULO** kwa upande wa Mamlaka za Maji za Wilaya na Miji midogo na **CHALINZE** kwa upande wa miradi ya kitaifa.

Mamlaka nyingine zilizofanya vizuri ni kama inavyofafanuliwa hapa chini:

i. Mamlaka za maji **MOSHI, MAKAMBAKO** na **KASHWASA** zilizofanya vizuri zaidi katika kufikia malengo ya kiutendaji katika utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira.
ii. Mamlaka za maji **SHINYANGA, MAGANZO** na **KASHWASA** zilizofanya vizuri katika kudhibiti upotevu wa maji.
iii. Mamlaka za Maji **MOSHI, IRINGA, DODOMA, MAKAMBAKO, USA-RIVER na DAKAWA** zimefanya vizuri katika uwasilishaji wa tozo ya udhibiti.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya **EWURA**, Bw. Ahmad Kilima amesema washindi hao kwa ujumla wamepatikana baada ya kushindanishwa kwa kutumia viashiria vya utendaji vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Ushindanishaji na Ulinganishaji wa Utendaji wa Mamlaka za Maji uliotolewa na EWURA mwaka 2018.

Aidha, Bw. Kilima amesema katika kuchukua tahadhari dhidi ya **COVID-19;** mamlaka zilizofanya vizuri zitapokea tuzo na vyeti kupitia ofisi za kanda za **EWURA** nchini kote ili kuepuka mkusanyiko tofauti na ilivyokuwa inafanyika katika miaka iliyopita kwa viongozi wa mamlaka zote kukutana kwenye mkutano wa mwaka.

**EWURA** ina kanda tano ambazo ni Kanda ya Ziwa, ambayo ofisi yake ipo Mwanza; Kanda ya Kaskazini (Arusha); Kanda ya Kati (Dodoma); Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya); na Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam.)

Bw. Kilima amesema kutokana na mabadiliko katika sekta ya maji, mamlaka za maji ambazo kwa sasa usimamizi wake umehamishiwa **RUWASA**, tuzo zao zitakabidhiwa kwa Mameneja wa RUWASA wa mikoa. Kwa mamlaka za maji ambazo zimeunganishwa na mamlaka zingine, tuzo zao zitakabidhiwa kwa mamlaka za maji zinazosimamia mamlaka hizo kwa sasa.

Bw. Kilima amesema **EWURA** itaendelea kuchukua hatua ili kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa mamlaka za maji na usafi wa mazingira nchini kwa lengo la kuziwezesha kutoa huduma kwa ufanisi.

Ripoti hiyo inapatikana katika tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz.

**Imetolewa na**
**MKURUGENZI MKUU**
**Dodoma**
**16/04/2020**

# Wenyeviti mbaroni madai kugeuza karantini biashara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara, inawashikilia wenyeviti wa vijiji wawili kwa tuhuma za kugeuza karantini ya corona biashara.

Wenyeviti hao wanatuhumiwa kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa watu ambao walitakiwa kuwekwa katika karantini.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa Takukuru mkoani Manyara, Isdory Kyando, wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya kukamatwa kwa wenyeviti hao.

"Katika ufatiliaji wa mienendo ya viongozi wenye dhamana ya kusimamia maagizo mbalimbali ya serikali ya kudhibiti maambukizi ya corona, Aprili 18, 2020 tuliwakamata viongozi wawili wa Kijiji cha Ngage," alisema Kyando.

"Katika hali ya kushangaza Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngage, Andrew Daniel na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ngage 'B', Letapuka Kuyani, pasipo kujali hatari ya corona kwao wenyewe, wakazi wa kijiji hicho na kwa Watanzania kwa ujumla wake na kutokana na tamaa ya fedha, walikuwa wanaomba Sh. 38,000 tu kwa kila anayetoka nje ya nchi kuingia kijijini humo ili wasiwaweke karantini.

Alisema viongozi hao walitaka wawape fedha hiyo na wawaruhusu waende kulala majumbani kwao.

Aidha, Kyando alisema wale ambao wamehifadhiwa kwenye karantini walikuwa wakiwatoza Sh. 28,000 kila mmoja kwa siku 14 wanazohifadhiwa, wakidai ni fedha za malipo ya madaktari na gharama za mafuta ya magari ya serikali pamoja na ulinzi, kitendo ambacho ni kinyume cha maelekezo ya serikali.

Kyando alifafanua kuwa, uchunguzi walioufanya umebaini kuwa watu walioingia nchini na kutakiwa kuwekwa karantini, lakini waliachiwa kwa kutoa rushwa, na kwamba ambao walikuwa wamewekwa karantini na kutozwa Sh. 28,000 waliingia nchini wakitokea Zambia, Kenya na Uganda.

Kwa mujibu wa Kyando, watuhumiwa wote wawili wanatarajiwa kufikishwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa.

"Uchunguzi wetu tumetambua na kubainisha majina ya watu ambao walipaswa kuwekwa karantini, lakini hawakuwekwa kwa misingi ya rushwa," alieleza.

Pia alisema majina ya watu waliokiuka taratibu yamekabidhiwa kwenye mamlaka husika ili zichukue hatua stahiki, na kuwaweka wahusika karantini huku taratibu za kisheria zifuate baadaye.

Aliwataka viongozi wa ngazi zote kufuata maelekezo ya serikali, badala ya kuangalia manufaa yao kwa gharama ya maisha ya Watanzania walio wengi.

# Kanyasu asema sekta ya utalii imeyumba

**Na Francis Godwin,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, amesema kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19, sekta ya utalii nchini imeyumba baada ya hifadhi nyingi kukosa watalii.

Amesema hali hiyo haijawahi kutokea Tanzania tangu ipate uhuru na kuomba Watanzania kuendelea kuliombea taifa na kutekeleza maagizo ya serikali kuhusu tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona.

Aliyasema hayo jana, wakati wa ziara yake kwa wananchi wa Wilaya ya Kilolo mkoani hapa, waliokumbwa na tatizo la tembo kuharibu mazao yao.

Kanyasu alisema amepokea ombi la wananchi wa Kijiji cha Irindi na Mbunge wa Kilolo, Venance Mwamoto, kuomba Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), kusaidia kukamilisha ujenzi wa jengo la sekondari ya kata ambalo limekwama kutokana na ukosefu wa fedha, lakini litakuwa gumu kutekelezeka kwa sasa kutokana na hali mbaya ya kifedha katika hifadhi hiyo.

"Sitaki kuwasemea Tanapa, naomba kueleza hali halisi ya hifadhi zetu kiuchumi kwa sasa kutokana na virusi hivi vya corona, hivi sasa hakuna wageni wanaotembelea hifadhi zetu kutalii zaidi ya wananchi wa kawaida wanaopita kwenye hifadhi zetu kuelekea makwao," alisema.

Alisema ameangalia taarifa ya Tanapa mwanzoni mwa mwezi huu, hakuwa na mtalii hata mmoja aliyeingia hifadhini.

"Hii haijapata kutokea toka nchi hii ipate uhuru, kwamba hakuna mtu hata mmoja ambaye ameingia Ngorongoro wala Serengeti zaidi ya Watanzania wanaopita na basi katika hifadhi hizo," alisema.

Kanyasu alisema ni wakati wa kila mmoja kuelekeza maombi kwa Mungu ili kuliepusha taifa na janga la corona ili maisha ya kawaida yaweze kuendelea na anaamini kuwa Mungu hana mpango wa kuangamiza Taifa la Tanzania wala kuangamiza dunia.

Vile vile, alisema wakati huu wa mpito wa virusi vya corona, Kamishna wa Tanapa kanda, anaweza kutembelea ujenzi huo ili hali itakaporejea kuwa nzuri kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wananchi ujenzi huo.

Katika hatua nyingine Kanyasu alisema, wizara yake inaendelea kufanya marekebisho ya fidia kwa wananchi watakaoharibiwa mazao yao na tembo ili serikali iwalipe kifuta jacho kikubwa tofauti na sasa mtu akiharibiwa shamba lake analipwa fidia ya Sh. 20,000 kwa heka.

## Lukuvi asaidia jimbo dawa za mil. 30/-

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MBUNGE wa Jimbo la Isimani wilayani Iringa, William Lukuvi, amekabidhi dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 katika vituo vyote na zahanati kwenye jimbo lake ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wake kipindi hiki cha janga la Covid -19.

Katibu wa Lukuvi, Thomas Malenga, akikabidhi msaada huo jana, kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Dk. Samwel Marwa, alisema msaada huo ni kwa ajili ya kusaidia wananchi wa jimbo hilo wanaofika katika vituo vya afya na zahanati kupatiwa huduma ya dawa badala ya kutumia fedha zao kwenda kununua katika maduka.

Alisema hatua hiyo imekuja kutokana mlipuko wa ugonjwa wa Covid -19 ambao umeendelea kusumbua dunia na kutokana na hali hiyo na uhalisia wa wananchi kiuchumi, ni wakati muafaka kuwasaidia dawa hizo na kupata huduma ya bure watakapokwenda kwenye vituo hivyo.

Akishukuru kwa niaba ya madiwani wenzake ambao vituo vyao vimepatiwa msaada huo, Diwani wa Kata ya Kising'a, Ritta Mlagala, alisema umefika wakati ambao wananchi wapo katika mazingira magumu ya kiuchumi kutokana na hofu ya virusi vya corona na wengi wao uwezo wa kwenda kununua dawa ni mdogo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Dk. Marwa alisema dawa hizo zimekuja wakati ambao wataalamu wa afya wapo kwenye mkakati na maandalizi ya kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid -19 na kuzuia maambukizi.

Alisema kuwa fedha ambazo serikali ilikuwa imezitenga kwa ajili ya ununuzi wa dawa kwa sasa zitaelekezwa katika matumizi mengine kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika zahanati na vituo vya afya.

# Ushirikiano Marekani, Tanzania, dunia mapambano dhidi Covid-19

SERIKALI ya Marekani inafanya kazi bega kwa bega na marafiki na washirika wake duniani kuhakikisha usalama wa afya duniani.

Msaada unaotolewa ni zaidi ya fedha na mahitaji. Wataalamu walioko duniani na wanaoendelea kutoa mafunzo kupitia mikutano ya kimtandao ni madaktari na wataalamu wa afya ya jamii, waliopata mafunzo kupitia ufadhili wa Marekani na taasisi zake za kielimu.

Ni mifumo ya ugawaji iliyowekwa wazi na inayoendelea kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa mahitaji ya dawa zinazohitajika, zenye ubora wa hali ya juu duniani. Marekani imetoa misaada ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha uhusiano na mataifa mengine duniani kwasababu inaamini ni jambo sahihi kufanya. Inafanya hivyo pia kwasababu majanga yanapotokea hayaheshimu mipaka ya nchi. Ikiweza kuzisaidia nchi kudhibiti milipuko ya magonjwa, itaokoa maisha ya watu ughaibuni na Marekani. Kwa Tanzania, dhamira ya Marekani ya pamoja kuhusu usalama wa afya haijawahi kuwa ya wazi na muhimu zaidi kuliko ilivyo sasa. Wataalamu wa maabara na wa afya ya jamii waliopata mafunzo kutoka Marekani, wanawapima washukiwa wa ugonjwa, wanawafuatilia waliokutana nao, wanabuni mikakati ya kujenga uelewa kwa wananchi na jitihada za mawasiliano hatarishi. Wataalam wa Marekani kutoka Taasisi ya Kimarekani ya Udhibiti wa Magonjwa (CDC), Shirika la Misaada na Maendeleo la Marekani (USAID) na Wizara ya Ulinzi, wanashauriana na wenzao wa Tanzania, kushughulikia msaada wa afya uliopo, na kuhakikisha kuna mwendelezo wa uhusiano huo, utakaojenga na kusaidia mfumo wa afya nchini Tanzania.

Uwapo wa pamoja wa ofisi za Taasisi ya Marekani ya Udhibiti wa Magonjwa (CDC) ndani ya Wizara ya Afya ni ukumbusho mzuri kwamba ushirikiano kwenye masuala ya afya uko kwenye kitovu cha uhusiano na Tanzania na watu wake. Dhamira ya Marekani kwenye ushirikiano huo bado iko imara, iliyojengwa kutokana na uwekezaji wa karibu Sh. trilioni 17.4 katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, zikiwamo zaidi ya Sh. 200,000 kwa kila Mtanzania aliye hai leo, katika kuunga mkono Sekta ya Afya nchini Tanzania.

Mwaka huu pekee msaada wa walipa kodi wa Marekani utatoa Sh. trilioni 1.2 kwa ajili ya kushughulikia VVU/Ukimwi, ikiwamo karibu Sh. bilioni 275 kwa ajili ya tiba ya kuokoa maisha ya dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi na bidhaa zingine za afya, wakati pia ikitoa ufadhili kwa ajili ya mishahara kwa baadhi ya wafanyakazi muhimu ambao ni nguvukazi ya Wizara ya Afya nchini kote.

Wakati uwekezaji wa Marekani nchini Tanzania ambao ni wa kiwango kikubwa na wa kudumu ni sehemu ya uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni 100 na imefanya kwa ajili ya afya ya waafrika barani kote katika kipindi cha miongo miwili iliyopita.

Katika kukabiliana na mlipuko wa Covid-19, dhamira ya Marekani kwa Marekani, kwa Africa na kwa afya ya dunia haijawahi na haitatetereka.

Tangu mlipuko wa Covid-19 serikali ya Marekani imetoa msaada wa Dola za Marekani milioni 500 hadi sasa duniani kote, zikiwamo Sh. bilioni 3.2 kwa ajili ya kusaidia juhudi za Tanzania.

Hakuna nchi itakayopambana na Covid-19 peke yake. Marekani itawasaidia wengine kwenye nyakati zao za uhitaji mkubwa. Itaendelea kuzisaidia nchi mbalimbali kujenga mifumo imara ya afya inayoweza kuzuia, kugundua, na kukabiliana na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza. Kwa pamoja inawezekana kuishinda changamoto hii ya kihistoria iliyoletwa na janga la Covid-19, kila siku, duniani.

**■Imeandikwa na Dk. Inmi Patterson, Kaimu Balozi wa Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wasanii, wachezaji nyota saidieni nchi janga corona

**TAKRIBANI** dunia nzima kwa sasa katika sekta ya michezo kimya kimetawala, hakuna mchezo wowote unaoendelea wala burudani kutokana na janga la virusi vya corona (COVID-19), ambavyo vinaendelea kuteketeza maelfu ya uhai wa watu duniani.

Hii ni kutokana na virusi hivyo vilivyoanzia China katika mji wa Wuhan kutokuwa na dawa wala kinga hatua iliyosababisha jumla ya watu 160,896 kupoteza maisha huku 2,340,539 wakiwa wameambukizwa hadi jana mchana duniani kote, hatua iliyosababisha mataifa mbalimbali kuzuia shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo na burudani, Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi iliyochukua hatua hiyo.

Lakini pia baadhi ya nchi zimefika mbali zaidi hususan za Ulaya, Asia na chache za Afrika kwa kuweka karantini ya watu kutoka nje, lengo likiwa ni kuzuia kasi ya maambukizi ya virusi hivyo vinavyoambukizwa pia kwa njia ya hewa.

Katika mataifa mengi hususan Ulaya wasanii wakubwa, wachezaji mastaa, matajiri, kampuni na watu wenye uwezo wa wastani kifedha wamekuwa wakijitoa kusaidia serikali zao kwa hali na mali katika kupambana na janga hili na si kuzisaidia serikali zao tu, bali wamejitoa hadi katika mataifa ambayo wanafanya kazi huko/wanacheza soka kwa kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia kupambana na corona.

Mfano wa kuigwa katika hilo ni mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowisk, ambaye yeye na mkewe wametoa euro milioni moja zaidi ya Sh. bilioni mbili za Tanzania kusaidia janga hilo, mwingine ni mshambuliaji wa Barcelona, Muargentina Lionel Messi na Kocha wa Manchester City, Mhispania Pep Guardiola kila mmoja akitoa euro milioni moja kuisaidia Serikali ya Hispania kupambana na janga hilo.

Wiki iliyopita mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Didier Drogba, naye alijitolea hospitali yake kubwa iliyopo nchini Ivory Coast kutumika bure kwa kuwa kituo cha matibabu ya wagonjwa wa COVID-19 katika kipindi hiki huku akigawa na vyakula, pia tumesikia namna wasanii wa muziki na wachezaji flamu na mastaa wengine nchini Marekani wanavyojitolea mamilioni ya dola kuisaidia serikali yao katika kupambana na janga hili linaloitesa dunia kwa sasa. Nipashe tunaamini misaada wanayotoa wasanii na wachezaji hao si kwamba wanazo fedha nyingi sana, bali wanaamini hiyo ndiyo njia pekee ya kurudisha fadhila kwa mashabiki wao ambao wamekuwa wakiwasapoti siku zote katika kazi zao.


Hivyo katika kipindi kigumu kama hiki ambacho mashabiki wao wanalazimika kufungiwa ndani na kushindwa kutoka kwenda kutafuta mkate wao wa kila siku, ni fadhila ya hali ya juu lakini pia ni msaada mkubwa kwa serikali yao.

Kama mashabiki wa soka hapa nchini wanaweza kuujaza Uwanja wa Mbagala Rangitatu kwa ajili ya kumsapoti Mbwana Samatta wakati akiicheza Aston Villa kule England na yeye kuvutiwa hadi kuiposti picha katika ukurasa wake wa Instagram, hii ina maana naye anapaswa kuwafanyia kitu hata kwa kugawa vitakasa mikono ['sanitizer'] angalau za laki tano tu kuonyesha yupo pamoja nao.

Si Samatta pekee bali wapo nyota wengi kama Simon Msuva hata wanaocheza soka la ndani mfano, Kelvin Yondani, John Bocco na wengine wengi wanaweza kufanya hivyo angalau hata katika vitongoji wanavyoishi kwa kugawa vitakasa mikono ama barakoa. Hatujawasikia pia wasanii kama Diamond Platinum ama Rajabu Abdul "Konde Boy" maarufu Harmonize, wakifanya hivyo katika jamii zinazowazunguka ama kwa kutoa moja kwa moja serikalini ili ziwafikie walengwa.

Tumefurahishwa na namna winga wa Simba, Francis Kahata, alivyogawa maji kwa jamii inayomzunguka kwao nchini Kenya wakati huu nchi yake ikipambana na janga la corona, hivyo tunaamini huo ni msaada mkubwa na kujitoa kwa hali ya juu kwa mashabiki na serikali yake jambo ambalo linapaswa kuigwa na wachezaji wa Tanzania na wengine wanaocheza Ligi Kuu pamoja na makocha wageni na wazawa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Sub' 5 zitaziangamiza timu ndogo Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**HIVI** majuzi, Kocha Mkuu wa Azam FC, Aristica Cioaba, aliliomba Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuongeza idadi ya wachezaji wa akiba kutoka watatu hadi watano ili kuwasaidia kujiepusha na majeraha hasa kwenye kipindi hiki cha janga la virusi vya corona (COVID-19).

Kocha huyo amesema kwa sasa kama Ligi Kuu ikirejea, wachezaji wengi huenda wasiwe na utimamu wa mwili kwa asilimia 100 kutokana na kufanyia mazoezi majumbani, hivyo huenda wakakumbwa na majeraha ya mara kwa mara na suluhisho ni kuongeza wachezaji watano wanaotakiwa kufanyiwa mabadiliko ['sub'] na isiwe watatu kama ilivyo sasa.

Akijibu maombi hayo, Mtendaji Mkuu wa Bodi la Ligi Tanzania, Almasi Kasongo, alisema kuwa itakuwa ngumu mno kubadili kanuni katikati ya msimu.

"Sijajua anaomba kwa sababu ya dharura ya changamoto hii ya COVID-19 tulionayo au vipi, lakini kama ni kulinda wachezaji na majeraha, labda tulichukue ili wakati wa uboreshaji wa kanuni zetu tuliwasilishe, lakini sioni kama kwa sasa inawezekana, lakini maana ya wazo na yeye ni mwalimu na ameona kuna faida ya hilo, basi wakati wa uboreshaji wa kanuni liwasilishwe na tutalifanyia kazi," alisema Kasongo.

Kwa hili mimi niko sehemu zote mbili kwa Cioaba na Kasongo, kwani kila mmoja ameeleza kutokana na jinsi alivyo kwenye nafasi yake.

Cioaba ametazama afya za wachezaji hasa watakaporejea uwanjani, lakini Kasongo ameangalia zaidi kwenye kanuni.

Ni kweli wachezaji watakaporejea, kwani baadhi yao hawatokuwa kwenye kiwango kile kinachotakiwa, hivyo makocha kuwa na uhuru mpana wa kuchagua na kutoa wachezaji hadi kufikia watano.

Lakini pia kwa sasa haiwezekani kwa sababu kanuni hutungwa kabla ya ligi kuanza na haiwezekani kuingizwa nyingine katikati au mwishoni mwa msimu.

> **Lakini pia kwa sasa haiwezekani kwa sababu kanuni hutungwa kabla ya ligi kuanza na haiwezekani kuingizwa nyingine katikati au mwishoni mwa msimu. Vyovyote itakavyokuwa, maoni au maombi ya Cioaba yanatakiwa yawasilishwe kabla ya kuanza kwa msimu ujao wa Ligi wa 2020/21.**

Vyovyote itakavyokuwa, maoni au maombi ya Cioaba yanatakiwa yawasilishwe kabla ya kuanza kwa msimu ujao wa Ligi wa 2020/21.

Hata hivyo, kama Bodi ya Ligi ikiingiza kanuni hii kwenye ligi hii inayoendelea, au msimu ujao inaonekana itakuja kuzinufaisha klabu zenye uwezo mkubwa wa kifedha wa kununua wachezaji wengi wenye uwezo.

Timu kama Azam, Simba na hata Yanga, zinaweza kunufaika na kanuni hii kwa sababu klabu zao zina uwezo wa kuwa na wachezaji wawili au watatu wanaocheza namba moja wenye uwezo unaofanana, hivyo akitoka huyu, akiingia ni kama aliyetoka.

Nadhani hata Cioaba ameliona hilo na ndiyo maana anataka wachezaji waongezwe ili hata wale ambao hawapati namba, lakini wana uwezo waweze kucheza.

Kanuni hii inaweza kuwa mwiba mchungu kwa baadhi ya timu ambazo hazina bajeti kubwa ya usajili na unaweza kukuta wachezaji 11 waliopo ndani labda na wengine wawili tu, ndiyo wana uwezo mkubwa, lakini waliobaki ni wa kujaza idadi tu.

Mfano timu kama Alliance FC ikitoa wachezaji tegemeo watano kwa sababu wamechoka uwanjani na kuwaingiza wengine, inacheza na Azam au Simba ambazo nazo zinatoa wachezaji waliocheza na kuingiza wengine watano, wenye uwezo mkubwa na nguvu mpya, fikiria nini kitatokea.

Ni kama vile mechi hiyo imeanza upya na zitakuwa na nguvu kubwa, kutokana na aina ya uwezo wa wachezaji wake. Ndiyo maana nasema kwenye kanuni hii Cioaba ameangalia zaidi faida ya timu yake na klabu zingine zenye uwezo wa kufanya usajili mzuri.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# HUDUMA ZA TRA KWA NJIA YA MTANDAO

**Ndugu mlipakodi TRA inakukumbusha kuwa, huduma zifuatazo zinapatikana kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika ofisini;-**

1. Usajili wa TIN unaotumia namba ya kitambulisho cha taifa,
2. Makadirio na malipo ya kodi ya majengo,
3. Kujisajili kwa ajili ya kufanya malipo ya kodi moja kwa moja kupitia mfumo wa Revenue Gateway System na GePG,
4. Kuwasilisha kadhia za forodha kupitia mfumo wa TANCIS,
5. Kikokotoo cha magari yaliyotumika na kununuliwa kutoka nje ya nchi,
6. Kikokotoo cha kodi za ajira,
7. Minada kwa njia ya mtandao,
8. Maulizo na uwasilishaji malalamiko katika kituo cha huduma,
9. Kuchapisha cheti cha kodi ya zuio,
10. Uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

**Kumbuka kuwa, unaweza kupata fomu mbalimbali kwa kutembelea tovuti yetu ya www.tra.go.tz**

**Kwa mawasiliano zaidi tufikie kwa kutumia mawasiliano yafuatayo;-**
**Simu za bure: 0800-750075 au 0800-780078**
**WhatsApp: 0744-233 333**
**Barua pepe: huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

# Fisi walivyojeruhi wanakijiji

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Ngogwa Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamenusurika kuuawa baada ya kushambuliwa na fisi wakati wakijaribu kumfukuza, alipovamia kundi la mbuzi.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Upendo Shirima, alisema tukio hilo lilitolea jana asubuhi, ambapo fisi huyo alivamia zizi la mbuzi kabla ya wananchi kuanza kumpiga na ndipo alipowashambulia wananchi sehemu za mikononi, huku baadhi walipelekwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Aliwataja walioshambuliwa ni Donald Simoni (27) na Furaha Ngusa (46), na kwamba wanaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kutenga siku maalumu ili kwenda kuwawinda fisi hao ambao wamekuwa wengi wakati huu.

"Tunaomba tu watu wa maliasili watusaidie kufanya oporesheni juu ya wananyama hao, maana kutokana na mvua hizi maji wameingia kwenye mapango yao, hali ambayo inawafanya waje kwenye makazi ya watu," alisema Shirima.

Alisema kuwa watu wameanza kupata hofu kutokana na wananyama hao kuanza kuvamia nyakati za mchana.

Diwani wa Ngogwa, Kamuli Mayuga, alisema baada ya kuwafikisha hospitalini walipatiwa matibabu kwa kushonwa nyuzi kwenye majeraha na kuruhusiwa kuerejea nyumbani.


Enabel

**Vacancy – Position no: 1708**

**Monitoring and Evaluation Technician in Kigoma Region**

***Enabel – Belgian Development Agency – recruits a Tanzanian national***

- Duty station: Kigoma town/district
- Contract term: 1 year – extendable – competitive salary package.
- Profile: Bachelor degree Information Technology, Agricultural economics, Records Management, Informatics, Computer Science or equivalent.
- Minimum experience: 1-year in data management
- Job content: mobile data Collection, People Management in Agricultural extension, Training, Data Analysis & visualisation, Reporting and Mapping.
- Competencies: Advanced user of Excel and good knowledge of monitoring and evaluation concepts; Experience in conducting qualitative/quantitative analysis integrating a gender perspective and/or a human-rights based approach, vulnerable groups or similar is a plus; Knowledge of ODK and GIS is an asset; Good reporting skills in English/ Kiswahili.

Details vacancy at: **https://btctanzania.wordpress.com/**
Submit your applications **mentioning the position number to: recruitment.tza@enabel.be**
**Deadline: 3rd May 2020**
Only shortlisted candidates will be contacted.

Female applicants are especially encouraged to apply. Enabel has zero tolerance for any form of discrimination and does not discriminate on the basis of HIV/AIDS status.

215707502


## Kanisa lapiga jeki hospitali vitimwendo 15

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HOSPITALI ya Wilaya ya Kibaha iliyopo Lulanzi, ambayo pia ni kituo cha kuhudumia wagonjwa wa Covid-19 imepatiwa msaada wa vitimwendo 15.

Msaada huo umetolewa na kanisa la Fellowship la jijini Dar es Salaam, ulikabidhiwa mwishoni mwa wiki kwa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya mji wa Kibaha.

Akikabidhi viti hivyo, Askofu Dk. Mgulu Kilimba alisema, lengo la kutoa viti hivyo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni nne, ni kusaidia jitihada za serikali kukabiliana na ugonjwa wa corona.

"Tatizo hili limekuja na litaondoka kwa kuwa Mungu anawapenda watu wake hivyo tukimlilia atalion-doa gonjwa hili na watu wataendelea na shughuli zao kama kawaida," alisema.

Aliwaomba Watanzania kuwaombea wahudumu wanaowahudumia wagonjwa wa Corona ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri huku wakichukua tahadhari. Alisema, wameshatoa vitimwendo hivyo zaidi ya 4,000 hapa nchini kwa kushirikiana na halmashauri na wabunge.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Tulitweni Mwinuka, alisema viti hivyo vitasaidia kuziba ukosefu wa vifaa vya hospitali na vifaa tiba.

Mwinuka alisema, kituo hicho ni moja ya hospitali zilizopewa fedha na serikali Sh. bilioni 1.5 na ilikamilika, lakini serikali ilikifanya kuwa kituo cha kuhifadhi wagonjwa wa corona baada ya tatizo hilo kutokea.


**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Tanzania Zanzibar na Mikoa ya Katavi, Rukwa, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani na Dar Es Salaam kuwa, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Pili utafanyika kwa siku tatu kuanzia tareh 02 hadi 04/05/2020.

Uboreshaji huu utafanyika katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika,Vituo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni
Uboreshaji Awamu ya Pili utafanyika kwa kuzingatia tahadhari zote za afya kuhusu kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na Virusi vya Corona.
Uboreshaji utafanyika kama ifuatavyo :-

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika tarehe 02-04/04/2020
2. **VITUO:** boreshajii Awamu ya Pili utafanyika katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika.
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha.**
- Kuandikisha Wapiga Kura wapya waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri huo ifikapo siku ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.
- kuandikisha wale wote ambao wana sifa lakini hawakujiandikisha katika Uboreshaji wa Awamu ya Kwanza..
- Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza kadi zao
- Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimeharibika
- Kuhamisha taarifa za wapiga kura waliohama kata au majimbo na kwenda katika maeneo mengine ya kiuchaguzi
- Kurekebisha taarifa za Wapiga Kura ambazo zilikosewa.
- Kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa kama vile waliofariki dunia.

**UTARATIBU WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA.**
- Katika kila kituo cha ofisi ya kata kutakuwa na Mwandishi Msaidizi na BVR KITs Operator ambao watakuwa na orodha ya vituo vyote katika Kata.
- Mwananchi ataweza kuandikishwa kulingana na kituo atakachopigia kura siku ya Uchaguzi Mkuu ndani ya Kata husika.
- Mpiga Kura yeyote anaweza kuboresha taarifa zake kwa kuzingatia kituo anachotaka kupigia kura siku ya Uchaguzi Mkuu.

**Muhimu:** Kumbuka kuzingatia Kanuni za Afya kwa kufuata Maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya Virusi vya Corona

Gerald G. J Mwanilwa
Kny; MKURUGENZI WA UCHAGUZI

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar Es Salaam, Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.**


# NEC mbioni kuhamia jengo jipya Dodoma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UJENZI wa ofisi mpya ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) jijini Dodoma, umefikia zaidi ya asilimia 90 na itakabidhiwa muda wowote kuanzia sasa.

Jengo hilo linajengwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (Suma JKT).

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Oparesheni wa Suma JKT, Meja James Philemon, alisema mteja wao atakabishiwa jengo hilo muda wowote na ujenzi wake umezingatia viwango vya hali ya juu.

"NEC watakabidhiwa jengo hili likiwa tayari kwa matumizi, mtakumbuka Suma JKT tulikabidhiwa mradi huu Januari mwaka huu, baada ya mkandarasi wa awali, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuonekana kushindwa kumudu kasi ya utekelezaji wa mradi huu," alisema.

Alifafanua kuwa, mkataba wa ujenzi wa Ofisi za NEC ulisainiwa Januari 7, ambapo utelelezaji rasmi ulianza Januari, mwaka huu.

Naye, Meneja wa mradi wa Suma- JKT, Mhandisi Lazaro Masanja, alisema ujenzi wa ofisi mpya za NEC umezingatia viwango vya hali ya juu, na kwamba mteja wao atakabidhiwa jengo imara.

Alisema mbali na jengo hilo lenye ghorofa nane, kuna majengo mengine mawili ya kisasa ambayo ni jengo la kutangazia matokeo liliowekewa ukumbi mkubwa kwa ajili ya wageni, viongozi, waangalizi wa uchaguzi pamoja na waandishi wa habari.

Mkuu wa JK, Brigedia Jenerali Charles Mbuge, alisema jeshi hilo limejipanga vyema kuhakikisha kuwa miradi yote linayoingia mikataba na wateja wote inakamilika kwa viwango vya hali ya juu na kukamilika kwa wakati.

Mbuge alisisitiza jeshi halijawahi kushindwa kazi, huku akisisitiza kuwa vijana wake wenye weledi wa hali ya juu walikuwa wanafanya kazi usiku na mchana katika maeneo yote ya miradi.

Tayari, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Charles Mahera, alishasisitiza kuwa Tume hiyo imejipanga kuhamia jijini Dodoma mara moja, baada ya kukabidhiwa jengo hilo.

Kwa mara ya kwanza NEC itatangazia matokeo yake ya uchaguzi mkuu katika ofisi zake mpya za Dodoma, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa NEC.



Mwenyejiti NEC, Jaji Semistocles Kaijage.

HABARI KITAIFA

# Mwanza waungana kulilia huruma ya Mungu

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WAUMINI wa madhehebu mbalimbali mkoani Mwanza wameshiriki maombi ya pamoja ya kumuomba Mwenyezi Mungu aondoe janga la corona na kufanya uponaji kwa waliopatwa na ugonjwa huo.

Akiongoza maombi hayo yaliyohudhuliwa na viongozi mbalimbali wa kidini na serikali akiwamo Mkuu wa mkoa huo, Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa Mwanza, Askofu Philipo Mafuja, alisema lengo la maombi hayo ni kuomba huruma na msaada wa Mungu aondoe janga la COVID-19, kutoshuka kwa uchumi sambamba na kuwaombea viongozi wote wa dini na serikali.

Alisema harakati mbalimbali zinafanyika ili kujilinda na kujiepusha na janga hilo, lakini kusimama katika imani na kumuomba Mungu ndio msingi mkubwa kwa kuwa yeye ndiye kimbilio na tumaini letu hivyo watu wote wanapaswa kubadilika na kuchukua tahadhari zote ili kupambana na gonjwa hilo.

"Kwa nini tunaogopa, Watanzania tusiogope hata kama idadi itaendelea kupanda tusirudi nyuma, bali tuendelee kusimama katika imani na kumuomba Mungu," alisema Askofu Mafuja.

Padre Faustine Bagwa , Mch. D. Jacob Mutash na Askofu Amos Hulilo ni baadhi ya watumishi wa Mungu waliotoa neno katika ibada hiyo na kusema wataendelea kutoa hamasa kwa waumini ili kujenga maarifa na hekima ili waweze kutenda yaliyo mema kwa kupenda kusali kwa pamoja pasipo kutengana.

Walisema wakati mataifa makubwa yakiamini sayansi pamoja na vifaa vya kujikinga na virusi vya corona, sisi mbali ya kutumia vifaa hivyo tutaushinda ugonjwa huo kwa maombi.

Mkuu wa mkoa huo, John Mongella, alisema kuna mahali tumemkosea Mungu, hivyo kupitia maombi yanayofanywa na waumini wa madhehebu mbalimbali hakika kutaipata huruma yake.

Pia aliwataka waumini hao kufuta maneno yaliyosemwa kuwa Afrika itakuwa kitovu cha corona, bali waungane katika maombi sambamba na kufuata, kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya.




Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, Sada Malunde, akipokea msaada wa madawati 60 na mabati 56 kwa Shule ya Msingi Biharamulo 'B', viti na meza 140 kwa shule za sekondari Kalenge na Katahoka, kutoka kwa Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa wa NMB, Amos Mubusi, wakati wa hafla iliyofanyika wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini madai kuingiliana kinyume cha maumbile

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Nkinda Shekalage (34), mkazi wa Tegeta Wazo jijini Dar es Salaam, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na mashtaka ya kuwaingilia wenzake watano kinyume cha maumbile.

Mshtakiwa huyo na wenzake walisomewa mashtaka mwishini mwa wiki mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, baada ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mkunde Mshanga, aliwataja washtakiwa wengine ni mwanafunzi Ahmad Mrisho (36), Gifti Emmanuel (20), mkazi wa Tegeta kwa Mboyo, Mwanafunzi Jackson Kiss (20), Christopher Songea (20) wakazi wa Gongolamboto, Salum Kachende (21) mfanyakazi wa ndani mkazi wa Tegeta na Mlinzi Ramadhani Mlekwa wa Manzese.

Jamhuri ulidai katika shtaka la kwanza mpaka la tano linamkabili mshtakiwa Shekalage kwa kuwaingilia kinyume na maumbile watu watano.

Mshanga alidai kati ya Januari 2017 na Machi, mwaka huu, Shekalage kwa nyakati tofauti alimwingilia Mrisho, Emmanuel, Kiss, Songea na Kandeche.

Katika shtaka la sita, ilidaiwa kuwa kati ya Januari 2004 mpaka Machi mwaka huu Mrisho alimruhusu Shekalage kumuingilia kinyume na maumbile wakati akijua ni kosa kisheria.

Pia, katika shtaka la saba, nane, tisa na la 10, mshtakiwa Emmanuel, Kiss, Songea na Kachende walimruhusu kuwaingilia kinyume na maumbile huku akijua ni kosa kisheria.

Shtaka la 11, ilidaiwa kuwa kati ya Januari 2019 na Machi, mwaka huu mshtakiwa Kiss anadaiwa kumwingilia kinyume cha maumbile Mlekwa wakati shtaka la 12 Mlekwa akidaiwa kuwa tarehe za tukio la 11, alimwingilia kinyume cha maumbile Kiss.

Mshanga alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, na aliomba mahakama kupanga tarehe ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Chaungu alisema dhamana iko wazi, lakini Hakimu aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo ana udhuru, hivyo Kesi yao itasikilizwa maelezo ya awali Mei 5, mwaka huu.

# NMB yazipiga jeki shule Biharamulo

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE tatu wilayani Biharamulo mkoani Kagera, zimepigwa jeki kutokana na changamoto za miundombinu.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, shule hizo zimepatiwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 15 ili wanafunzi wake wasomee katika mazingira rafiki.

Benki ya NMB ndiyo iliyosaidia uwezeshaji huo, ambapo vifaa vilivyotolewa ni pamoja na mabati 56 na madawati 60 kwa ajili ya Shule ya Msingi Biharamulo' B', viti na meza 140 kwa shule za sekondari za Kalenge na Katahoka zote za wilayani humo

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Kaimu Meneja wa benki hiyo Kanda ya Ziwa, Amos Mabusi, alisema msaada huo ni sehemu ya faida ya benki hiyo ambayo hurudisha kwa jamii kwa kuchangia miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu , afya na pale yanapotokea majanga.

Mabusi alisema katika kurudisha fadhila kwa wananchi, benki hiyo imetenga kiasi cha Sh. bilioni moja kwa mwaka 2020 kwa ajili ya miradi ya maendeleo huku kipaumbele kikiwa ni kusaidia sekta ya elimu na afya

"Kiasi hiki kinaweza kuonekana si kikubwa sana, lakini kimekuwa msaada mkubwa kwa jamii hasa katika sekta ya afya na elimu vifaa kwenye sekta hizi mbili zimekuwa ni changamoto kubwa katika hospitali, vituo vya afya pamoja na shule zetu hapa nchini, " alisema Mabusi. "Vitu hivi tulivyokabidhi leo ni moja ya ushiriki wetu katika maendeleo ya jamii na sisi kama benki tunahakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika kutokana na faida tunayoipata," alisema Mabusi.

Aidha alisema benki hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu wamewafikia zaidi ya vijana 41,781 kupitia program yao ya "jifunze, jipange, wajibika" inayotolewa kwa shule za msingi na sekondari nchini iliyolenga kuwafundisha vijana umuhimu wa kuweka akiba na mipango kwa ajili ya maendeleo yao na kukidhi mahitaji muhimu.

Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo, Sada Mahunde, alisema benki ya NMB imekua ikichangia mara kwa mara misaada katika wilaya hiyo, na kwamba uamuzi wa benki ya NMB kuchangia sekta ya elimu ni kichocheo kikubwa cha kuingia kwenye uchumi wa viwanda.

Sada alisema wilaya hiyo ina changamoto kubwa za miundo mbinu za samani katika sekta ya elimu na afya, na kuziomba taasisi nyingine kuiga kutoka benki hiyo ili kushiriki kutatua changamoto zilizopo.

# Malori mbaroni tuhuma kubeba vifaa vya mgodi

**Na Mohab Dominic,** KAHAMA

MALORI 11 yamekamatwa na Jeshi la Polisi Kituo cha Kagongwa wilayani Kahama mkoani Shinyanga na Polisi Maswa mkoa wa Simiyu yakidaiwa kubeba vifaa vya mgodi wa Buzwagi vilivyokuwa vikipelekwa Mgodi wa North Mara Tarime mkoani Mara.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea juzi mchana na kuongeza kuwa ofisi yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kituo cha Kagongwa walikamata magari hayo, huku mengine matano yakizuiwa yalipokuwa njiani wilayani Maswa mkoani Simiyu.

Kumburu alisema vifaa hivyo ni vile vilivyozuiwa na Wizara ya Madini wakati wa kufanyika mnada na kutakiwa kusubiri maelekezo ya serikali.

Alifafanua kuwa, kati ya magari hayo, sita yalikamatwa na askari wa kituo cha Polisi Kagongwa na magari mengine matano yalikamatwa na askari wa kituo cha Polisi Maswa mkoani Simiyu.

Alieleza kuwa wakati wa ukamataji huo magari mengine matatu yalizuiwa kutoka ndani ya Mgodi wa Buzwagi, na kusema kuwa magari hayo yalikuwa yanasafirishwa na Kampuni ya Mainline Carriers ya jijini Dar es Salaam.

"Vifaa hivyo ni vilivyobebwa na malori hayo pamoja na dumper bucket kwenye magari matano, na vifaa mbalimbali vya Dumper kama vile difu, matairi, madigadi, rejeta na matairi," alisema Mhandisi Kumburu.

Alisema kuwa malori hayo yalisafirishwa bila ya kupewa ridhaa ya Serikali kama walivyoelekezwa, na kuongeza kuwa kutokana na hali hiyo, wamewaelekeza vifaa hivyo visisafirishwe hadi hapo watakapotekeleza maelekezo ya Serikali.

Kumburu alisema licha ya kukamata malori hayo, pia alifanya mawasiliano na Meneja Mkuu wa Mgodi wa Buzwagi na Bulyanhulu, Benedictor Busunzu, ambaye alitoa ushirikiano.

# RC achukizwa waziri kudanganywa corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA.

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amechukizwa na kitendo cha mkazi wa mkoa huo, Mussa Kisinza (25), wa kijiji cha Mwakitolyo wilaya ya Shinyanga, kwa kumpigia simu Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, na kumdanganya kuwa ana maambukizi ya virusi vya corona.

Telack alibainisha hayo Ijumaa wakati akikabidhiwa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya corona, kutoka kwenye kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu Barrick kupitia mgodi wake wa Buzwagi, ambao ulikabidhi matenki ya maji, barakoa, vipima joto, dawa, groves na mavazi ya madaktari.

Alisema hakupendezwa na kitendo cha mtu huyo kumpigia simu waziri, na kumdanganya kuwa ana maambukizi ya corona na wakati hana virusi hivyo, na kuwa kitendo hicho ni mzaha dhidi ya janga hilo.

Hata hivyo, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kumkamata ili achukuliwe hatua kali za kisheria.

"Natoa onyo kwa wakazi wote wa mkoa wa Shinyanga, yeyote yule ambaye atapuuza maagizo ya serikali na kulifanyia mzaha janga hili la virusi vya corona, tutamkamata na kumchukulia hatua," alisema. "Nawapongeza pia wadau kwa kuendelea kushirikiana na Serikali kupambana na virusi vya corona mkiwamo Barrick, kwa kutoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi haya, na mkoa wa Shinyanga hakuna mshukiwa hata mmoja wa corona wala watu kukaa karantini," aliongeza.

Mkuu wa kitengo cha Afya na Usalama Kazini, Dk. Antoinette George, kutoka Barrick kupitia mgodi wake wa Buzwagi wilayani Kahama, alisema wametoa msaada wa vifaa hivyo vya kujikinga na virusi vya corona kutokana na kinga kuwa bora kuliko tiba.




Waziri Mkuu wa Afya, Ummy Mwalimu, akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Songas, Anael Samuel (wa kwanza kulia), ukiwa ni mchango wa kampuni hiyo kusaidia mapambano ya ugonjwa wa homa ya virusi vya corona (Covid 19). Makabidhiano hayo yalifanyika katika ofisi za Waziri Mkuu, Dar es Salaam, juzi. Wa pili kulia ni Meneja Rasilimali Watu wa Songas, Agatha Keenja na wa kwanza kushoto ni Ofisa Mkuu wa Fedha, Sebastian Kastuli **PICHA: NA MPIGA PICHA WETU**

# TPSF, wadau kukabili athari za corona

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imewataka wazalishaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumika kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, ikiwamo barakoa, kuongeza uzalishaji zaidi ili kukidhi mahitaji ya soko nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki mara baada ya kutembelea kiwanda kinachozalisha barakoa cha Open-Sanit jijini Dar es

Salaam, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema sekta binafsi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wameona ipo haja ya kuhamasisha wajasiriamali kutumia fursa hii kuzalisha zaidi ili kukabiliana na athari za ugonjwa huo.

"Mahitaji ya barakoa yamekuwa makubwa ili kukabiliana na kuenea kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID-19), hivyo TPSF imeona ichukue nafasi hii kuwahamasisha wajasiriliamali kuzalisha kwa wingi bidhaa hiyo katika kipindi hiki kigumu," alisema. Katika kuitumia fursa hivyo, TPSF wamefanya mazungumzo na Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ili waweze kutumia majengo ya mamlaka hiyo yalipoyopo barabara ya Kilwa.

"Wajasiriamali wengi husument wanaohusika na mambo ya urembo na ubunifu wamekuwa waathirika wakubwa na uwepo wa ugonjwa huu hali ambayo imewaathiri sana kiuchumi, tupo katika mazungumzo na wenzetu wa TANTRADE ili kuona namna ya wajasiriamali wadogo watakavyoweza kuyatumia majengo hayo ili waweke mashine zao na kuanza uzalishaji wa barakoa," alisema.

Alisema sababu ya kutumia majengo haya yanakidhi miongozo ya kiafya hasa katika kipindi hiki cha kukabiliana na COVID-19, lakini pia mazingira ya eneo hilo ni mazuri na yenye utulivu mkubwa.

"Tunaamini ombi letu litakubaliwa hasa ukizingatia kwa sasa taifa zima tumeungana na kuwa kitu kimoja, eneo hilo la sabasaba ni kubwa na linakidhi maelezo ya wataalam kutoka Wizara ya afya na pia lipo katika uzio," alisema na kuongeza kuwa hali hiyo itaongeza ajira na mapato kwa mtu mmoja mmoja na serikali kwa ujumla. Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara Tanzania (TNBC), Dk. Godwill Wanga, alisema wajasiriamali lazima wawe wabunifu katika suala zima la uzalishaji wa bidhaa hasa katika kipindi hiki.

"Ubunifu unahitajika kwa wenye viwanda ili kutumia fursa kama hizi katika kunusuru afya ya Watanzania na kuchangia ukuaji wa uchumi," alisema Dk. Wanga

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Octovian Mshiu, alisema kumekuwa na changamoto ya uzalishaji wa bidhaa hiyo kutokana na uhitaji mkubwa ukilinganisha na uwezo wa uzalishaji kwa sasa.

"Uzalishaji wetu kwa wiki ni barakoa 22,000, hii ni changamoto kubwa ukilinganisha na mahitaji ya Watanzania zaidi ya milioni na tano, tupo tayari kutoa uzoefu wetu katika kuunga jitihada za Serikali na TPSF kwa ujumla," alisema Bw. Mshiu.

Nipashe
Spotika



CAVANI NI SASA EPL AU KAMWE? UK. 12 & 13



Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, akikwamisha mpira wavuni dhidi ya kipa wa Everton, timu hizo zilipokutana msimu huu.

## ISIKUPITE

BEKI wa kati wa Real Madrid, Sergio Ramos, ndiye mchezaji wa pili katika historia ya klabu hiyo kuweza kutwaa mataji mengi (21), akiwa nyuma ya Paco Gento, anayeshikilia rekodi ya kubeba mataji 23 na miamba hiyo ya Santiago Bernabeu.

# KLABU 4 ANAZOWEZA KUTUA AUBAMEYANG

**LONDON,** England

HUKU Pierre-Emerick Aubameyang akiingia mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake, Arsenal inaweza kulazimika kumuuza nyota wake huyo.

Aubameyang amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu alipojiunga na Arsenal, huku mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon akifunga mabao 61 katika mechi 97 alizocheza hadi sasa. Arsenal walilipa euro milioni 65 kumsajili yeye kutoka Borussia Dortmund na mshambuliaji huyo wa sasa analipwa kiasi cha pauni 200,000 kwa wiki.

Mkataba wa sasa wa Aubameyang pale Arsenal unamalizika mwishoni mwa msimu huu na kama watashindwa kufikia makubaliano ya kumpa mkataba mpya watalazimika kumuuza kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon atafikisha umri wa miaka 31 miezi michache ijayo na inaweza kuwa nafasi yake ya mwisho kupata mkataba mkubwa. Pia anataka nafasi ya kushinda mataji kabla hajastaafu kucheza soka.

Huku Arsenal wakiwa wanakijenga kikosi chao upya chini ya kocha Mikel Arteta, klabu inataka kuwa kwenye ushindani wa kuwania mataji.

Makala haya yanaangalia klabu nne anazoweza kusajiliwa Aubameyang:

### #1. REAL MADRID

Wakati Luka Jovic na Mariano Diaz hawapo kwenye kiwango kizuri pale Real Madrid hadi sasa wakiwa na mshambuliaji mmoja pekee, Karim Benzema, kocha Zinedine Zidane atakuwa anaagalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji mpya kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Aubameyang ni mmoja wa washambuliaji bora duniani na bila shaka raia huyo wa Gabon akiwa anakaribia kufikisha umri wa miaka 31, atakuwa anataka kumaliza kipindi chake cha uchezaji akiwa kwenye klabu kubwa, mshahara mkubwa pamoja na uwezekano wa kutwaa mataji. Real Madrid wanaweza kumpata kwa muktadha huo.

Kwa mujibu wa ripoti, Zidane ameshabainisha kwamba ana nia ya kumleta Aubameyang pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu, huku yeye akiwa chaguo la pili kwa sababu kipaumbele chao ni Erling Haaland. Hata hivyo, haitakuwa kazi rahisi kwa Borussia Dortmund kumuachia mshambuliaji wao huyo mpya ambaye atakuwa amekaa kwao kwa kipindi cha miezi sita tu.

Hivyo, kumsajili Aubameyang utakuwa usajili sahihi kwa Real kwa sasa. Los Blancos wataweza kufikia ada yake na mshahara wake wa wiki, hasa ukichukulia kiwango chake cha kufunga mabao kinaweza kuipa taji Real Madrid miaka inayokuja.

### #2. BARCELONA

Mpango wa Barcelona kumuwania Aubameyang unaonekana kama umekufa kwa siku za hivi karibuni, lakini wakati wa dirisha la Januari hadi Machi, miamba hao wa Hispania walionekana wana nia kubwa ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Arsenal.

Huku Antoine Griezmann, Ousmane Dembele na usajili mpya wa Martin Braithwaite hatima zao zikiwa hazijulikani, Barcelona wanaweza kurudi tena kwa nyota huyo wa Gabon. Ingawa kipaumbele cha Barcelona kwa kipindi kinachokuja cha majira ya joto ni Neymar, lakini huwezi kuondoa uwezekano wa kumtaka Aubameyang.

Kwa mujibu wa ripoti, mshambuliaji huyo wa zamani wa Dortmund ameonyesha nia yake ya kutaka kucheza pale Barcelona, hivyo anaweza kucheza pamoja na Lionel Messi. Na kama wataonyesha nia ya dhati kumhitaji, Arsenal wanaweza kumuuza.

Kama ilivyo kwa Real Madrid, Barcelona wana uwezo wa kufikia ada ya kumnunua pamoja na mshahara atakaoutaka Aubameyang hautakuwa tatizo kwao.

### #3. PARIS SAINT-GERMAIN

PSG nao wameonyesha nia ya kutaka kumsajili Aubameyang na anaweza kuwa mtu muhimu zaidi kwao.

Huku Neymar bado akijaribu kulazimisha uhamisho wa kuondoka pale kwenye mji mkuu wa Ufaransa, Edinson Cavani naye akitaka kuondoka pamoja na Mauro Icardi kumalizika kipindi chake cha kucheza kwa mkopo, kocha Thomas Tuchel atalazimika kusajili mshambuliaji mpya kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Fedha si tatizo kwa PSG na kama Aubameyang anataka kujiunga na klabu hiyo atakuwa na kumbukumbu nzuri, kwani alishawahi kuichezea AS Saint-Etienne na kurudi kwake tena Ufaransa itakuwa kumbukumbu ya kuvutia.

Aubameyang amejithibitishia yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora duniani na baada ya kuonyesha kiwango chake kwenye ligi ngumu duniani, atakuwa na wakati mzuri wa kupata changamoto mpya kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, ambayo pengine inaweza kuwa si yenye kutumia nguvu zaidi kama Ligi Kuu ya England.

### #4. MANCHESTER UNITED

Nafasi ya Aubameyang kujiunga na Manchester United inaweza kuwa ndogo sana, lakini kwenye soka lolote linaweza kutokea, hasa ikikumbukwa kwamba, Arsenal waliwahi kumuachia Robin van Persie ajiunge nao. Usajili mara zote unakuwa usiotabirika kwenye dunia ya soka na ndio maana United wamepewa nafasi ya kumsajili.

Manchester United kwa sasa inatafuta mshambuliaji na majina mengi yametajwa kuhusika nao akiwamo Aubameyang.

Kwa mujibu wa ripoti, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon anaweza kuwa chaguo sahihi zaidi kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya England.

## Extra Time



# CAVANI NI SASA EPL AU KAMWE?

**LONDON,** England

EDINSON Cavani amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora katika kizazi chake huku akiwa na kiwango kisichoshuka cha kufunga mabao kwa klabu na nchi yake. Lakini katika umri wake wa miaka 33, anatakiwa sasa kuamua uhamisho wake wa mwisho katika maisha yake ya soka kama anataka kubaki kwenye kilele cha juu.

**Ligi Kuu ya Italia, Serie A na ile la Ufaransa, Ligue 1, imefurahia kiwango bora kabisa cha raia huyo wa Uruguay akiwa katika klabu za Napoli na Paris Saint-Germain. Amepewa tuzo ya shujaa katika klabu zote. Ingawa staili yake ya uchezaji, nguvu na uwezo wake dimbani bado unaonyesha kuna mengi zaidi kwake kabla ya kutundika daluga.**

Chakushangaza, ubora wake unafiti kabisa kwenye soka la Uingereza, lakini kamwe hajawahi kucheza kwenye Ligi Kuu ya England, licha ya mara kwa mara kuhusishwa na kuwaniwa na klabu kubwa za EPL. Jose Mourinho aliripotiwa kumuwania Cavani akiwa Chelsea wakati wa kipindi chake cha pili katika klabu hiyo mwaka 2013. Lakini walikuwa ni PSG ndio waliofanikiwa kuipata huduma yake.

Pamoja na kuwa na kiwango cha kuvutia na bora zaidi, lakini Cavani ameshindwa kuisaidia klabu hiyo kuwa na mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, mashindano ambao wamekuwa wakiyasotea kwa muda mrefu sasa. Na hali hiyo kwa vyovyote haiwezi kubadilika hivi karibuni. Amefanikiwa katika kila kitu kwa mashindano ya nyumbani kwenye klabu hiyo kwa misimu saba. Ripoti za hivi karibuni zimebainisha kwamba, sasa unaweza kuwa muda wake wa kuondoka.

Jina la Cavani litavutia ofa nyingi kutoka Mashariki ya Kati, Mashariki ya mbali na Marekani. Lakini, hayupo tayari kucheza kwenye levo za chini ambapo anajua kwamba bado ana uwezo wa kucheza ligi kubwa. Wakati anakwenda Paris alivutiwa na kutaka mafanikio Ulaya ambayo pale Napoli hakuweza kuyapata. Hata hivyo, amebaki kuwa kwenye mshangao licha ya majina makubwa kumfuata lakini hawakupata mafanikio.

Cavani alitua Serie A katika klabu ya Palermo akitokea nyumbani kwao Uruguay mwaka 2007. Kwa miaka mingi, amejiimarisha yeye mwenyewe kuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa katika soka la kisasa. Ana taswira ya gwiji kwenye timu yake ya Taifa. Zaidi ni kwamba, kuna uhusiano wa karibu kati ya wanasoka wa Amerika Kusini na Napoli ukianzia kwa Diego Maradona.

Kuna utamaduni na mtazamo sawa pale mjini Naples, unaowavutia na kuwafiti wachezaji wa Amerika Kusini. Na kuanzia hapo kwenye dimba la San Paolo ndipo wanapoanza kupata mafanikio na kutengeneza njia ya kwenda katika klabu nyingine kubwa zaidi Ulaya. Cavani alichukua changamoto hiyo na kuja kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi pale Napoli.

### SHUJAA WA TAIFA

Cavani mara zote amekuwa na rekodi bora kabisa ya kufunga mabao katika kipindi chake chote cha uchezaji. Mafanikio yake yamezidiwa tu na mshambuliaji mwenzake wa timu ya Taifa, Luis Suarez, ambapo kumemfanya kutopata tuzo binafsi nchini mwake. Hata hivyo, Cavani anatambulika na kuheshimiwa na mashabiki pamoja na wachambuzi, ambao wanatambua zaidi mchango wake kwa timu kuliko takwimu zake binafsi.

Thamani hiyo imemuwezesha Cavani kufurahia mafanikio ya muda mrefu katika uchezaji wa daraja la juu, na yupo tayari kuonyesha kwenye Ligi Kuu ya England nini ambacho wamekuwa wakikikosa. Ni mchezaji ambaye yupo fiti, mshambuliaji mwenye nguvu na ubora ambao unaweza kung'ara zaidi kwenye soka la Uingereza.

Uwezo wake wa kufunga hauna maswali, zaidi ya mabao 300 chini ya mechi 600 za Klabu. Ana mabao 50 kwenye mechi 100 za kimataifa akiwa na kikosi cha Uruguay. Mkongwe wa mashindano makubwa sita, yeye ni mtu ambaye atapewa heshima kubwa na mashabiki wengi wakati wa kustaafu kwake, wakati takwimu zake binafsi zitakapoingia kwenye historia pamoja na staili yake ya uchezaji.

Bila shaka, Ligi Kuu ya England inahitaji mtu wa umri wake, licha ya ufiti wake. Uwezo wake utakuwa muhimu zaidi kwa timu atakayotua. Anaweza kuwa mpango B wa kubadili mchezo kwa timu yoyote na pia kiongozi bora zaidi kwa wakati mmoja.

### KUJITUMA KLABUNI

Ripoti ya kutopewa nafasi pale kwenye kambi ya Paris Saint-Germain itauliza maswali juu ya morali yake. Kwa nyongeza kuanza mradi mpya kwenye soka la Uingereza katika hatua hii inaweza kumfanya kuanza kuwa na majukumu mapya. Muda wake akiwa Napoli na Paris Saint-Germain ulionyesha yeye ni mtu ambaye anajiwekeza kwenye klabu yake kwa muda mrefu. Lakini muda haupo tena upande wake.

Mtu aliyekuwa anavutiwa naye zaidi wakati wa utoto wake alikuwa ni mshambuliaji wa zamani wa Argentina, Gabriel Batistuta, na Batigol alikuwa mmoja wa wachezaji aliyetengeneza jina lake kule Serie A bila kucheza Ligi Kuu ya Uingereza. Baada ya misimu saba, ni wazi kwamba muda wa Cavani pale Paris umefikia mwisho. Kusimama kwa ligi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kutampa muda muhimu zaidi wa kufanyia mahesabu ya wapi atakwenda kumalizia soka lake.

### NJAA YA UEFA

Mshindi wa Copa America akiwa na Uruguay mwaka 2011, na sehemu ya kikosi cha Paris Saint-Germain kilichotawala soka la Ufaransa, bado Cavani hajatimiza ndoto yake. Atakuwa anajivunia nama alivyoiwakilisha klabu na alivyojitolewa kwao katika zama zake. Lakini muda huu ni wa kuangalia hisia zake binafsi.

Cavani atakuwa na hamasa kubwa ya kubeba taji la Ligi Kuu ya England na ana nafasi kubwa zaidi ya kufanikiwa kule. Kiukweli ni wachezaji wachache sana katika levo yake, na umri wake ambao wanakuwa bado wako fiti dimbani na kuweza kukabiliana na changamoyo yoyote. Inaweza pia kuwa ni nafasi yake ya kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufanikiwa kwenye ligi na michuano ya kimataifa.

## Nukuu

"Ukweli mimi ni shabiki wa Arsenal si siri, [ila] sina upendeleo wowote wapi wachezaji wanakwenda, sijaribu kumlazimisha yeyote kutoka klabu moja kwenda nyingine. Kila kitu ni uwezekano, Ligi Kuu England ni kitu ambacho [Philippe Coutinho] mara zote anafurahia kucheza hapo, na ninapenda acheze hapo, na pengine angependa kurudi na kucheza hapo," **wakala wa Coutinho, Kiavash "Kia" Joorabchian.**



"Ni kama nipo pale; Nafikiri kuhusu mazoezi na timu, unafikiria vibaya, lakini kamwe sijawahi kuwaza hivyo, mara zote nakuwa kwenye hali ya kawaida, inanifanya niwe na njaa ya kurudi na kufanya vizuri, na hiyo inanionyesha namna gani napenda soka," **Paul Pogba akieleza nia yake ya kurejea mapema dimbani.**



"Sina taarifa kama Ivan Rakitic anataka kuondoka na hajawasilisha ombi hilo kwangu. Na kwa upande wangu amecheza kwa muda mwingi na kwa kiwango kizuri na anaendelea kufanya hivyo. Nina furaha na kiwango chake na sina cha kusema, tunatakiwa kusubiri na kuona nini kitatokea na kama anataka kuondoka au la. Na kama natakiwa kusema hivyo, muda utakuja," Kocha wa Barcelona, Quique Setien





EDINSON Cavani amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora katika kizazi chake huku akiwa na kiwango kisichoshuka cha kufunga mabao kwa klabu na nchi yake. Lakini katika umri wake wa miaka 33, anatakiwa sasa kuamua uhamisho...

Uk. 12&13



Straika wa Simba, Meddie Kagere, akishangilia moja ya mabao yake kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam msimu huu. Kagere ameweka rekodi ya kufunga mabao manne peke yake kwenye mechi moja dhidi ya Singida United, timu yake ikishinda mabao 8-0. **PICHA: MAKTABA**

# NYAVU UWANJA WA UHURU ZILIVYOGEUKA KINARA KWA MATOBO

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Ligi Kuu duniani kote zikiwa bado kwenye karantini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara zinaonyesha Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ndiyo uliozalisha mabao mengi mpaka sasa.

**Uwanja huo unaonekana ni hatari kwa timu za mikoani zinapocheza na timu zingine kubwa za Dar es Salaam, lakini pia kwa timu ambayo haijajipanga vema.**

Pamoja na kwamba si mkubwa kama Uwanja wa Taifa, lakini takwimu zinaonyesha kuwa ndiyo uwanja uliozalisha mabao mengi kwenye mechi moja msimu uliopita na msimu huu.

Mei 8, mwaka jana, msimu uliopita wa Ligi Kuu, Simba iliichakaza Coastal Union mabao 8-1 kwenye Uwanja wa Uhuru na kuwa ndiyo mechi iliyofungwa magoli mengi zaidi kwa msimu huo.

Machi 11, mwaka huu, Simba iliiadhibu Singida United mabao 8-0 kwenye uwanja huo huo, na mechi hiyo pia mpaka ligi inasimama, inashikilia rekodi ya kufungwa magoli mengi kwenye mchezo mmoja.

Mpaka sasa Uwanja wa Jamhuri Dodoma ndiyo unaoshikilia rekodi ya kuzalisha mabao machache zaidi.

Wakati tayari mabao 284 yamefungwa mpaka sasa kwenye ligi, ni matano tu yamefungwa kwenye uwanja huo ambao kwa sasa unatumiwa na JKT Tanzania kama uwanja wa nyumbani.

Mwandishi wa makala haya ameorodhesha viwanja 10 ambavyo vinaongoza kwa kutinga mabao mengi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**1. UWANJA WA UHURU (MABAO 77)**

Ni uwanja unaoongoza kwa kuruhusu mabao mengi kwenye milingoti yake. Jumla ya mabao 77 yameshatinga vyavuni. Ukiachana na kutumiwa na timu kongwe za Simba na Yanga ambazo mara nyingi hupenda kuutumia vema, lakini sababu nyingine ni kwamba msimu huu timu ya Azam FC imekuwa ikiutumia kama uwanja wa nyumbani kutokana na uwanja wake wa Azam Complex kuwa kwenye matengenezo. Kama vile haitoshi, timu ya KMC inautumia pia kama uwanja wa nyumbani pamoja na Ruvu Shooting na JKT Tanzania.

**2. UWANJA WA SAMORA (MABAO 58)**

Uwanja wa Samora uliopo Iringa, unakamata nafasi ya pili kwa kuruhusu mabao 58 mpaka sasa. Ni uwanja unaotumiwa na Lipuli ya Iringa ambayo kwenye mzunguko wa kwanza ilikuwa ikishinda kwa idadi kubwa ya mabao timu zinapokanyaga hapo.

Sababu nyingi inaoufanya uwanja huo kuwa na mabao mengi ni timu za Prisons na Mbeya City ambazo kuna wakati zilihamia huko na kuufanya uwanja wao wa nyumbani, kutokana na Uwanja wa Samora kuharibiwa na mashabiki kwenye tamasha la muziki.

**3. UWANJA WA TAIFA (MABAO 56)**

Uwanja Mkuu wa Taifa jijini Dar es Salaam unakamata mafasi ya tatu kwa kuruhusu idadi kubwa ya mabao. Umezidiwa mawili tu na Uwanja wa Samora, kwani mabao 56 yametinga nyavuni kwenye uwanja huo.

Hata hivyo, kuna wakati uwanja huo haukuwa unachezewa mechi nyingi za ligi msimu huu, hasa mzunguko wa kwanza.

**4. UWANJA WA CCM KIRUMBA (MABAO 34)**

Ni uwanja unaotumiwa na timu za Mbao FC na mechi chache za Alliance, hasa inapocheza na timu za Simba na Yanga. CCM Kirumba inakamata nafasi ya nne kwa kutengeneza mabao mengi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ambapo tayari mabao 34 yametinga nyavuni.

**5. UWANJA WA KAITABA (MABAO 31)**

Jumla ya mabao 31 yamefungwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba ambao unatumiwa na timu ya Kagera Sugar kama uwanja wake wa nyumbani.

Unakamata nafasi ya tano kwa kuruhusu mabao mengi kwenye ligi msimu huu mpaka sasa, kwa mabao 31 kutumbukia kwenye kamba.

**6. UWANJA WA SOKOINE (MABAO 29)**

Jumla ya mabao 29 yametinga nyavuni kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya na kushika nafasi ya sita, licha ya kwamba kuna wakati timu zenyewe Prisons na Mbeya City zilihamishwa hapo kutokana na uwanja huo kuharibika wakati wa tamasha la muziki. Inawezekana kabisa ungekuwa juu zaidi ya hapo kama mechi zote za timu hizo zingechezwa katika dimba hilo.

**7. UWANJA WA MAJALIWA (MABAO 28)**

Ni uwanja ambao wenyeji Namungo FC wanauita 'machinjioni'. Unakamata nafasi ya saba kwa kuruhusu mabao 28, moja tu pungufu ya Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya. Ni uwanja mpya kabisa ambao msimu huu ndiyo umeanza kutumika kuchezewa Ligi Kuu.

**8. UWANJA WA NYAMAGANA (MABAO 27)**

Unaweza usiamini hili, lakini ukweli ndiyo huo kuwa Uwanja wa Nyamagana Mwanza uko kwenye 10 bora ya viwanja vilivyoruhusu mabao mengi mpaka sasa. Unatumiwa na Alliance FC ambao mzunguko wa kwanza ilifanya vizuri, lakini kipigo cha mabao 5-0 dhidi Azam FC Novemba 26, mwaka jana, kiliongeza idadi kubwa ya mabao.

**9. UWANJA WA MKWAKWANI (MABAO 24)**

Kwa sasa Coastal Union iko vizuri na hata kwenye msimamo inakamata nafasi ya nne, hivyo uwanja wake kuwa kwenye 10 bora ya vilivyoruhusu mabao mengi wala haishangazi.

**10. UWANJA WA NANGWANDA SIJAONA (MABAO 22)**

Uwanja wa Nangwada Sijaona unafunga dimba ya viwanja vilivyoruhusu mabao mengi kwenye Ligi Kuu. Mabao 22 yamefungwa kwenye uwanja huo unautumiwa na Ndanda FC kama wao wa nyumbani. Kumbuka kuwa jumla ya viwanja 22 vinachezewa Ligi Kuu msimu huu.

**JE, WAJUA?**

KLABU ya Simba ya jijini Dar es Salaam, bado inashikilia rekodi ya kuwa klabu ya kwanza barani Afrika kuweza kupindua matokeo kwa ushindi mkubwa ugenini kwenye Klabu Bingwa Afrika [Kwa sasa Ligi ya Mabingwa] baada ya mwaka 1979 kukubali kipigo cha mabao 0-4 nyumbani dhidi ya Mufurira Wanderers ya Zambia, kabla ya kwenda ugenini na kushinda 5-0, mabao yote yakifungwa na wachezaji wawili; Thuwen Ally (hat-trick) na George "Best" Kulagwa aliyetupia mawili, wakati huo ikinolewa na kocha shabiki na mwanachama wa Yanga, marehemu Joel Nkaya Bendera. Na kipigo hicho ikikitoa mbele ya Rais wa Zambia wa wakati huo, Kenneth Kaunda.



# DC abaini mazingira hatarishi kujikinga corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobasi Katambi, amewaagiza wamiliki wa hoteli na baa jijini Dodoma, kufuata maelekezo ya serikali ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Katambi alitoa agizo hilo, katika kikao cha pamoja na wamiliki hao, kilichofanyika mwishoni mwa wiki Ofisini kwake, baada ya kufanya ziara kwenye maeneo ya starehe jijini hapa.

Alisema wamiliki hao wanapaswa kuhakikisha watu wanaoingia kupata huduma katika sehemu hizo wanakuwa salama kama zilivyokuwa sehemu nyingine.

Pia, katika ziara yake baadhi ya maeneo amebaini hali isiyoridhisha ya watu kujikinga na ugonjwa huo.

"Nawaomba mfuate maagizo yaliyotolewa la sivyo tutawafungia msitoe huduma kwa jamii inayowazunguka, wengi wenu mmeonekana kupuuzia," aliwaonya.

Alisema sheria lazima zifuatwe na kila mmoja ili kuwaweka wananchi salama.

"Naomba watu mfuate masharti sheria haichagui mtu yeyote atakayekiuka lazima atakamatwa,"alisema Katambi.

Alisema Ofisi yake itaendelea kuzunguka kuangalia nani anakiuka taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona ambao ni tishio hivi sasa duniani kote.

"Hivi sasa Dodoma ipo salama hivyo ni vema watu tukaendelea kufuata masharti ili jiji letu liendelee kuwa salama kutokana na umakini wa viongozi wa kusimamia watu wananawa mikono kila wanapoingia sehemu zenye watu," alisema.



Diwani wa Chamwino, Jumanne Ngede, akionyesha taka za vifungashio vya majani ya migomba, zilizotupwa katika dampo la soko la Bonanza jijini Dodoma, ambazo zimepigwa marufuku na Halmashauri ya Jiji la Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

## KKKT yaongeza ibada kwa watu wazima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KANISA Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dodoma, limesitisha kwa muda ibada ya watoto na kuongeza ibada za watu wazima huku muda wa kusali ukipunguzwa.

Hayo yalisemwa jana na Mchungaji kiongozi wa Usharika huo, Venance Maunga, wakati akihubiri kanisani hapo.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kupunguza mikusanyiko ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya serikali.

Pia alisema ibada ya watoto kanisani hapo imesitishwa hadi hapo hali ya nchi itakapokuwa shwari kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, aliwataka wazazi kuendelea kuwafundisha watoto hao wawapo nyumbani ili wasisahau waliyokuwa wanafundishwa.

"Kuanzia sasa (jana) ibada ya watoto haitakuwapo, kwenye ibada za watu wazima tumepunguza muda wa kusali, kila ibada tutakuwa tunasali saa moja, ibada hizo zitakuwa kaunzia saa 12 asubuhi hadi saa tano asubuhi,"alisema.

Alisema hali hiyo itapunguza watu kukaa muda mrefu kanisani pamoja na watu kuwa wengi.

"Kuna vitu vingi vya kutosha ambavyo waumini mnaweza kuvitumia bila kusogamana,"alisema.

Katika ibada hiyo watu walikaa kwa kupeana nafasi huku wazee wa kanisa wakionekana kila wakati kusimamia watu wanaosogeleana na kuwapa elimu ya kukaa kwa nafasi.

Pia, kanisa linapigwa dawa kabla na kila baada ya ibada ikiwa ni tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona.

# Bakwata yaonya maimamu, walimu misikitini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) wilayani Dodoma, imewaonya Maimamu na Walimu wa misikiti na vyuo vya madrasa watakaogundulika kuwakusanya watoto kwenye majengo yao, watachukuliwa hatua kali ikiwamo kuwafuta nyadhifa zao.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa halmashauri ya Baraza Kuu la Bakwata, wilayani hapa, Ustadhi Bashuru Hussen, alipokuwa akizungumza na viongozi na waumini wa msikiti wa Imani West Chinangali, jijini Dodoma.

Bashuru alisema kuwa, kuendelea kukusanya watoto hao kwenye misikiti ni kukaidi maelekezo ya serikali pia wanaweza kuonekana wanasaidia kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema kuwa Mufti Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania, tayari alishatoa angalizo katika kipindi hiki cha uwapo wa ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kufuta masomo ya watoto wanaofundishwa kwenye madrasa zote ndani ya misikiti na vyuo vya dini ya kiislamu.

"Halmashauri Kuu la Baraza la Waislamu Dodoma mjini, kamwe haitawavumilia walimu na maimamu ambao watakaokaidi maagizo hayo ya serikali ikiwamo na Mufti Mkuu, na kwa yeyote atakayebainika atalazimika kuachia nafasi hiyo na hakuna haja yoyote ya kuinyooshea Bakwata au serikali," alisema.

Aliwataka viongozi wa baraza hilo wa wilaya hiyo kutoa elimu jinsi ya kujihami na ugonjwa huo kwenye maeneo yao kuanzia majumbani wanakotoka.

Alisema ugonjwa wa corona unawezekana kuondoka, lakini ni pale viongozi wa taasisi pamoja na wananchi wenyewe watakaposhirikiana kwa pamoja kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali kuhusu kuepukana na maambuzi.

Hivi karibuni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alibaini kuwapo kwa baadhi ya misikiti na makanisa kukusanya watoto kwa malengo ya kutaka kuwafundisha mafundisho ya kiroho wakati serikali ilishapiga marufuku mikusanyiko hiyo.





## Hati za kimila 10,837 zatolewa

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

JUMLA ya hati za kimila 10,837 zimetolewa kwa wananchi na ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Adhi mkoani Mbeya kwa lengo la kuwawezesha kuwa na umiliki halali wa ardhi.

Hayo yalibainishwa na Kamishina Msaidizi wa ardhi mkoani Mbeya, Jeremiah Minja, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mpango mkakati wa kuwawezesha wananchi kuwa na hati miliki.

Minja alisema hati za kimila zina umuhimu sana katika maisha ya kila siku ya wananchi kwa kuwa inamwezesha mwananchi kuwa na umiliki halali na kuweza kuaminika kirahisi na taasisi za kifedha kwa lengo la kupata mikopo.

Alisema kwa mjibu wa takwimu za mwaka kuanzia Julai, 2019 hadi Machi mwaka huu, ofisi ya ardhi mkoa wa Mbeya imegawa hati za kimila 10,837 kwa wananchi katika maeneo tofauti ya mkoa. Akitolea mfano, Minja alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini, jumla ya hati za kimila 9,879 zimegawiwa kwa wananchi, hati 732 zimegawiwa katika Halmashauri ya Mbarali na hati 129 zimegawiwa katika Halmashauri ya Rungwe.

Pia, alisema katika Halmashauri ya Busokero jumla ya hati 57 zimegawiwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuna hati 38 zilizogawiwa na katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ni hati mbili zilizogawiwa.

Alisema kuna baadhi ya halmashauri ambazo zimefanya vizuri kutokana na jitihada zao binafsi zikiwamo za kuwahamasisha wananchi kuwa na hatimiliki pamoja na kushirikiana na baadhi ya mshirika yasiyo ya kiserikali katika kufikia lengo la serikali la wananchi kuwa na hatimiliki.

Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini, Lembris Laizer, alisema hatua ya halmashauri hiyo kufikia lengo kubwa la kugawa hati za kimila inatokana na jitihada na mipango mikakati binafsi ya halmashauri ikiwamo elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na hatimiliki.

# Amri ya RC kufunga baa saa 3 usiku yatenguliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imetengua amri yake kwa wamiliki wa maeneo yanayofanya biashara ya vileo (baa) kuyafunga maeneo hayo kila siku saa 3:00 usiku kama njia mojawapo ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Utenguzi wa amri hiyo ulitangazwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, juzi, siku moja baada ya kutoa amri hiyo iliyokuwa imeambatana na amri ya wananchi kuacha kuzurura mitaani baada ya muda huo.

Chalamila alitengua amri hiyo baada ya kufanya mazungumzo na wamiliki wa baa na kuridhishwa na mikakati ambayo wamejiwekea kwa ajili ya kukabiliana na janga la corona.

Mwenyekiti wa wamiliki wa baa mkoani hapa, Heri Chaula, alisema wamejipanga kukabiliana na ugonjwa huo kwenye maeneo yao ya biashara ili kuepuka kusambaa na kuathiri biashara zao pamoja na shughuli za watu wengine.

Chaula alisema moja ya mikakati waliyokubaliana ni kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa na bilauri (glass) ambazo zikishatumika na mteja mmoja hazitatakiwa kutumika tena na badala yake zitatupwa na kila mteja atakuwa na yake.

Alisema pia watahakikisha katika maeneo yao kunakuwa na umbali wa mita moja kati ya mteja na mteja ili kuepuka kugusana ama kubadilishana hewa, hali ambayo inaweza ikasababisha kuambukizana ugonjwa huo.

"Lakini pia tumekubaliana kuwa kila mmiliki wa baa atakuwa na mtaalamu wa kuhamasisha matumizi ya vitakasa mikono ili watu wote wawe na uelewa na elimu itakuwa inatolewa kama watu hawajaelewa," alisema Chaula.

Vilevile, alisema kumbi zote za mziki na maeneo yote ya starehe yatafungwa kwa muda muafaka ili kuungana na serikali katika kukabiliana na janga la corona.

Baada ya maelezo hayo, Chalamila alisema mikakati hiyo ni mizuri na itasaidia juhudi za serikali za kukabiliana na ugonjwa huo, hivyo akatengua agizo lake la kufunga maeneo hayo saa 3:00 usiku. Alisema maelezo ya wamiliki hao yanaonyesha kuwa hawapingi uamuzi wa serikali, badala yake wamejiongeza na kubuni mbinu mbadala za kukabiliana na janga hilo.

"Kuanzia leo natengua rasmi amri ya kufunga maeneo haya saa 3:00 usiku na narejesha utaratibu wa awali ambao upo kisheria, sheria zimeainisha kila eneo linatakiwa kufungwa muda gani ila hakikisheni mnazingatia muda ulioainishwa kisheria," alisema Chalamila.

Aliwataka wamiliki hao kutekeleza kwa vitendo mikakati waliyoibuni ili kushirikiana na Serikali kukabiliana na janga la corona na kwamba kuna utaratibu Serikali itajiwekea wa kutembelea maeneo hayo usiku ili kuona kama maazimio hayo yanatekelezwa.

Vilevile aliwatoa hofu wananchi wa Mkoa huo kuhusu ugonjwa huo na badala yake akawataka kila mmoja kuchukua tahadhari kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba (kushoto), akimpatia maelezo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuhusu ujenzi wa stendi ya mabasi ya Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipotembelea mradi huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TFS kujenga barabara za kisasa kukuza utalii Kusini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, unakusudia kujenga miundombinu ya kisasa zikiwamo barabara katika vivutio vya Ziwa Ngosi mkoani mbeya na kwenye maporomoko ya Kalambo mkoani Rukwa ili kukuza utalii.

Hayo yamebainishwa na Meneja Msaidizi msimamizi rasilimali wa TFS, Kanda ya Nyanda za Juu kusini, Innocent Lupembe, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na mikakati mbalimbali ya kukuza utalii ziwa Ngosi na katika Maporomoko ya Kalambo.

Alisema uamuzi wa TFS kujenga miundombinu katika ziwa Ngosi na katika maporomoko ya Kalambo unalenga kuchochea utalii hususani utalii wa ndani na kuongeza mapato ya serikali.

Lupembe alitaja miongoni mwa miundombinu itakayojengwa katika ziwa Ngosi ambalo ni la pili kwa ukubwa katika Afrika kuwa ni barabara yenye urefu wa Km 7.2 itakayojengwa na wakala wa barabara vijijini na mijini(Tarura), vyoo vya kisasa na sehemu ya kituo maalum kwajili ya taarifa mbalimbali kuhusiana na ziwa hilo.

"Unajua ujenzi huu wa barabara hii ya Km 7.2 hadi ziwa ngosi utaanzia katika eneo la Igawilo kadi kwenye eneo linalotenganisha hifadhi ya Ziwa Ngosi na makazi ya wananchi na hii itasaidia kukuza utalii wa ndani na kuongeza pato la serikali," alisema.

Pia alisema katika maporomoko ya Kalambo ambayo ni ya pili kwa urefu katika Afrika baada ya maporomoko ya Tugera yaliyopo Afrika Kusini kutakuwa na ujenzi wa barabara, vyoo vya kisasa na sehemu ya kuweka mahema kwa watalii watakaokuwa wakitembelea.

Alisema fedha za ujenzi wa miundombinu hiyo katika maporomoko ya Kalambo na Ziwa Ngosi zinatokana na ufadhili wa shirika la Global Environment Facility (GEF), ambalo limetoa fedha hizo ili kuboresha miundombinu katika maeneo hayo kwa lengo la kuchochea utalii wa ndani.

Alisema ofisi ya TFS kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe na Rukwa, imejipanga kuhakikisha vivutio vya maporomoko ya Kalambo yaliyopo mkoani Rukwa na Ziwa Ngosi lililopo mkoani Mbeya vinakuwa na tija kwa maendeleo ya taifa.

# Wagonjwa wa corona Zanzibar wafikia 58

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imethibitisha wagonjwa wapya 23 waliogunduliwa kuwa na homa kali ya corona na kufanya idadi sasa kufikiya 58, huku wagonjwa wawili wapya wakitoka katika kisiwa cha Pemba. Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, alisema hayo katika taarifa yake kwa waandishi wa habari ambapo alisema watu 21 ni raia kutoka Tanzania, huku watu wawili ni raia wa kigeni.

Alisema kwamba mmoja aliyetambuliwa kuambukizwa na ugonjwa wa corona ni raia wa Cuba ambaye anaishi Zanzibar, huku mwengine ni raia wa Ufaransa. Mohamed alisema kwamba hadi sasa watu watatu wamefariki dunia waikiwamo wawili ambao walifariki majumbani.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ikiwamo kutoa taarifa mara wanapobaini dalili za ugonjwa huo ikiwamo kikohozi kikali pamoja na homa na mafua.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawataka wananchi kuchukua tahadhari kuhusiana na ugonjwa wa corona, ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na sababu. Taarifa fupi ya Wizara ya Afya hata hivyo, haikutaja wagonjwa wengine walioambukizwa na ugonjwa wa corona wanatoka katika mitaa gani katika mji wa Zanzibar.



Wananchi wakinawa mikono kabla ya kuingia katika Soko la Samaki Feri Dar es Salaam jana ikiwa sehemu ya utaratibu uliowekwa kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa Corona jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ZBC: Wanaowazushia kashfa viongozi wa SMZ kudhibitiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Utangazaji Zanzibar (ZBC), imesema itawachukulia hatua kali za kisheria wamiliki wa mitandao ya jamii pamoja na vyombo vya habari na utangazaji watakaobainika kurusha taarifa za uzushi zenye kusababisha taharuki kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mtendaji ZBC, Omar Said Ameir, wakati akizungumza na vyombo vya habari kuhusu kuwapo kwa taarifa za uzushi na uongo zinazowahusu viongozi wakuu wa Serikali.

Alisema Tume imepewa mamlaka kwa mujibu wa sheria kuona kwamba vyombo vya habari, vikiwamo vya utangazaji na mitandao ya kijamii inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Alieeleza katika siku za hivi karibuni, kumejitokeza baadhi ya wamiliki wa mitandao ya kijamii kuwachafulia viongozi wakuu wa nchi majina yao kwa malengo ya kisiasa.

Alisema Tume imesikitishwa na kitendo cha kumzushia Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, kuwa amemuingiza mgeni na kumpitisha katika chumba cha wageni maalumu bila ya kufanyiwa uchunguzi ikiwamo vipimo vya afya.

"Hizo taarifa zilizochapishwa katika mtandao mmoja nchini sio za kweli...siku hiyo waliyoandika katika mtandao huo waziri alikuwa nje ya nchi...ni taarifa zenye kutaka kuwachafulia watu majina yao na vyeo vyao," alisema.

Aidha, alisema katika siku za hivi karibuni, mtandao mmoja wa kijamii umekuwa ukichapisha taarifa za viongozi na kuwahusisha na mbio za urais wa Zanzibar, huku zikiwachafua majina yao na kashfa ambazo sio za kweli.

"Mawaziri Mohamed Ramia , Mohamed Aboud pamoja na Haji Omar Kheir wamechafuliwa majina yao kwa kuzushiwa kashfa mbali mbali...mitandaoni hiyo tutaidhibiti," alisema.

Aliwatahadharisha watu wengine kuacha kupokea taarifa za uongo na kuzisambaza, wajuwe hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Alisema wakati taifa lipo katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona sio vizuri hata kidogo kutoa taarifa za uzushi zenye kuleta taharuki kwa jamii.

Amer alisema tayari Tume imewasiliana na Jeshi la Polisi Zanzibar kwa ajili ya kuchukuwa hatua zaidi na kupambana na watu wa aina hiyo.

"Tume ya Utangazaji Zanzibar tayari tumetoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kuhusu hatua zaidi za kuchukuwa pamoja na Mamlaka ya mawasiliano nchini (TCRA)," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Awadh Juma Haji, alisema Jeshi la Polisi linachunguza na kuwatafuta watu wanaojihusisha na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii nchini kwa kutoa taarifa za udanganyifu zenye kusababisha taharuki kwa jamii.

"Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi zaidi na kuwatafuta watu wanaotumia vibaya mitandao ya jamii kutoa taarifa na kuwachafulia majina viongozi wa nchi," alisema.

# Maimamu waliokaidi agizo la Mufti waonywa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Wete Pemba, Khamis Mwadini Khatib, ametoa onyo kali kwa maimamu wa misikiti mbalimbali Pemba kwamba watachukuliwa hatua za kisheria kama wataendelea kukaidi agizo la Ofisi ya Mufti kuhusu masharti ya kufanya ibada ya Sala ya Jamaa.

Khatib alisema hayo wakati akizungumza na maimamu huko Pemba, baada ya kuwapo kwa taarifa kwamba, baadhi ya misikiti wamekaidi agizo la Ofisi ya Mufti kuhusu utaratibu wa kufanya ibada.

Alisema agizo la Ofisi ya Mufti linawataka Waislamu kufanya ibada ya sala ya pamoja (jamaa) huku watu wakiacha nafasi mita moja na nusu ikiwa ni sehemu ya tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Alisema baadhi ya misikiti agizo hilo wanalipinga na kutumia utaratibu wa zamani wa kushikamana kwa pamoja katika ibada zote za pamoja misikitini.

"Maimamu tuache tabia ya kupinga maagizo ya Ofisi ya Mufti ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kufuata mambo yote yanayohusu dini ya kiislamu....agizo hilo linatakiwa kutekelezwa ikiwa ni sehemu ya kujikilinda na ugonjwa wa corona," alisema.

Sheikhe Iddi Juma, imamu wa Msikiti wa Wete, alisema wamelipokea agizo hilo na watalitekeleza kwa sababu nchi inakabiliwa na janga la corona.

"Msikiti wetu pamoja na maamuma wote wamelipokea agizo hilo na tunalitekeleza kwa sababu ndiyo njia pekee ya kujilinda na ugonjwa wa corona," alisema.

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na gazeti hili, agizo la Mufti la kuwataka waumini wa dini ya kiislamu wakati wa kufanya ibada ya pamoja kuacha nafasi mita moja na nusu baina mtu mmoja na mwengine limewagawa waumini wengi.

Baadhi ya misikiti waumini wake wamekataa kuweka utaratibu wa kutoa nafasi kati ya mtu mmoja na mwengine huku wakisema kuacha nafasi kunaifanya ibada hiyo kuwa batili.

"Agizo la misikiti kuweka nafasi limewagawa waumini katika maoni tofauti...wapo wengine wanasema hakuna sababu ya kuweka nafasi kwani kufanya hivyo ni kubatilisha ibada yote," alisema Ali Issa, muumini anayesali katika Msikiti wa Mikunguni.

TANGAZO

# LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12. 2019

**Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | | 31-Dec-19 Iliyokaguliwa | 31-Dec-18 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 411 | 726 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 3,011 | 4,113 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 200 | 1,465 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 6 | 229 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 25,656 | 28,918 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,017 | 3,276 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za Udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,061 | 1,339 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **33,362** | **40,066** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 550 | 3,400 |
| 18 | Amana za Wateja | 9,525 | 11,397 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | 0 | - |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | 0 | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 473 | - |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | 0 | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 87 | 123 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,755 | 852 |
| 28 | Madeni | 8,094 | 9,224 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **20,484** | 24,996 |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **12,878** | 15,070 |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 38,457 | 38,048 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (22723) | (23282) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2856) | 304 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | 0 | |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **12,878** | **15,070** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 5,457 | 5,843 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,562 | 8,281 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 39% | 38% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 17.9% | 15% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 369% | 251% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77% | 72% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 105% | 86% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -32% | 0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -17% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA INAYOISHIA 31.12.2019

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | *(Kiasi kwa shilingi '000)* | 31-Dec-19 Iliyokaguliwa | 31-Dec-18 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 8,400 | 10,271 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,724) | (2930) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 6,676 | 7,341 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (3,489) | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | 2,872 | (417) |
| 6 | **Mapato yasiyo na Riba** | 800 | 1756 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (96) | (16) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 811 | 1221 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 85 | 551 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba** | (8112) | (8376) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (4391) | (4522) |
| | 7.2 Gharama nyingine | (3721) | (3855) |
| 8 | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | (1253) | 304 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (1603) | (36) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2856)** | **268** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumulisha (bainisha) | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **(2856)** | **268** |
| 13 | **Idadi ya Waajiriwa** | 145 | 169 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | N/A | N/A |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | N/A | N/A |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | **5** | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -8% | 1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | -10% | 1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 62% | 86% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 24% | 25% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | (Kiasi kwa shilingi '000) | 31-Dec-19 Iliyokaguliwa | 31-Dec-18 Iliyokaguliwa |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,253) | 304 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | | |
| | -Hasara Katika Mali za Kudumu | 1,517 | 2,288 |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,385 | (4,095) |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,909) | (1,138) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za muda mfupi | | |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 286 | (900) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 389 | 2,071 |
| | -Kodi iliyolipwa | 38 | (36) |
| | -Mengineyo | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | 453 | (1,507) |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawiwo Lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (40) | (253) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | (40) | (253) |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Madeni ya Muda Mrefu | 700 | 2,284 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawiwo Lililipwa kwa Fedha Taslimu | (972) | 737 |
| | Mengineyo | (2,006) | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (2,278) | 3,020 |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,865) | 1,260 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka | 5,575 | 4,315 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka | 3,710 | 5,575 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019

(Kiasi kwa millioni shilingi )

| Mwaka wa Sasa 2019 | Mtaji wa Hisa | Mtaji utokanao na hisa za upendeleo | Tengo la Ziada ya Jumla | Ziada ya Kisheria | Hasara Kusanyiko | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **29,237** | **8,520** | **291** | **-** | **(23,014)** | **15,034** |
| 1 Mapatao mengine yaliyojumuishwa | 700 | - | - | - | - | 700 |
| 2 Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (291) | - | 291 | - |
| 3 Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 4 Mengineyo - ( IFRS -9) | - | - | - | - | - | - |
| 5 Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | - | (2,837) | (2,837) |
| 6 Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| 7 | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **29,937** | **8,520** | **-** | **-** | **25,579** | **12,878** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 29,237 | 6,236 | 283 | 211 | (17,220) | 18,747 |
| 1 Mapatao mengine yaliyojumuishwa | - | 2,284 | - | - | - | 2,284 |
| 2 Transfer to general Provision reserve | - | - | 9 | - | (9) | - |
| 3 Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | (211) | 211 | - |
| 4 Ziada Ya Kisheria | - | - | - | - | (6,264) | (6,264) |
| 5 Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | - | - | - | - | 268 | - |
| 6 Mengineyo | - | - | - | - | - | 268 |
| 7 | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **29,237** | **8,520** | **291** | **0** | **(23,014)** | **15,034** |

| **Imesainiwa na:** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Andrew Tarimo<br>**(Mkurugenzi Mtendaji)** | | 31.03.2020 |
| Lydia Machangu<br>**(Meneja wa fedha na utawala)** | | 31.03.2020 |
| Rashid Sendoro<br>**(Mkaguzi wa ndani)** | | 31.03.2020 |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka sasa,

| **Imesainiwa na:** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Simon Jengo<br>**Mwenyekiti** | | 31.03.2020 |
| Godfrey Mramba<br>**Mkurugenzi** | | 31.03.2020 |

Sisi, tuliotajwa hapo juu, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.

HABARI KITAIFA

# Brela yaokoa mil. 63/- ya pango

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), unatarajia kuokoa Sh. milioni 63 ilizokuwa ikilipa kwa ajili ya ofisi yake kila mwezi baada ya kukabidhiwa jengo lililokuwa Makao Makuu ya Magereza.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa Oktoba 6, mwaka jana, akiwa ziarani mkoani Rukwa kwa kutaka taasisi na mashirika yote ya serikali kuondoka kwenye majengo binafsi na kuhamia kwenye majengo ya serikali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyaisa, alikabidhiwa jengo lililokuwa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza na Kamishna wa Magereza, Uwesu Ngarama, aliyemwakilisha Kamishna Jenerali wa Magereza (CGP), Suleiman Mzee.

Makabidhiano hayo yalifanyika kwenye jengo lililokuwa Makao Makuu ya Ofisi za Magereza lililopo karibu na makutano ya Sokoine na Mtaa wa Shaaban Robert, Dar es Salaam.

Akizungumza katika makabidhiano hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Nyaisa alisema, hatua inayofuata sasa ni kuwakabidhi jengo Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya ukarabati na baadaye taratibu za kuhamia zitafanyika.

Pia, Nyaisa aliishukuru serikali kwa kuipatia Brela jengo hilo ambalo litasaidia kuipunguzia taasisi matumizi makubwa ya fedha iliyokuwa ikitumia kwa kulipia pango.

"Kwa kipindi kirefu Brela imekua ikitumia fedha nyingi kulipia kodi ya pango katika jengo binafsi, mathalani baada ya kuhamia katika jengo hili Brela itaokoa zaidi ya shilingi za Kitanzania milioni 63.2, ambazo zilikuwa ikitumika kulipia kodi ya kila mwezi," alisema Nyaisa.

Oktoba 6, 2019 akiwa mkoani Rukwa, wakati wa uzinduzi wa barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga, Rais Magufuli alisema taasisi na mashirika ya serikali yamekuwa yakitumia fedha nyingi kulipa kodi katika majengo binafsi.

"Majengo ya serikali yapo lakini taasisi na mashirika ya serikali wamepanga kwenye majengo binafsi, kwa watakao endelea kubaki katika majengo hayo wahakikishe wanasababu za kuridhisha," alisema Rais Magufuli.

# Stamico wanolewa kuhusu corona

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO), limeungana na taasisi nyingine za umma na binafsi nchini katika kuwaasa wafanyakazi wake kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID -19).

Katika kufanikisha hilo, uongozi wa STAMICO uliandaa mafunzo ya siku moja yaliyofanyika kwenye viunga vya wazi vya ofisi hiyo kwa ajili ya wafanyakazi wake waliopo Dar es Salaam ambapo, pamoja na mambo mengine, walihimizwa kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa COVID 19 na kutakiwa kuripoti kwenye vituo vya afya vilivyoteuliwa mara waonapo dalili za ugonjwa huo.

Wafanyakazi hao waliambiwa kuwa kupata huduma ya afya mapema kutawaepusha na athari kubwa zinazoweza kutokea kutokana na maambukizi.

Taarifa iliyotolewa na STAMICO imesema mafunzo hayo yalilenga pia kuwatahadharisha wafanyakazi dhidi ya magonjwa mengine yanayoambukiza kwa njia ya virusi kama homa ya ini (Hepatitis B) na Ukimwi (HIV-AIDS).

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Bahati Mwasse, alinukuliwa na taarifa hiyo akisema maeneo ya kazini ndipo wafanyakazi wanapokutana kwa muda mrefu zaidi, hivyo kuwa kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa hayo.

"Dk. Mwasse aliwahimiza wafanyakazi wa STAMICO kuwa makini na kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi wetu wa Serikali, kama vile kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kunawa mikono mara kwa mara na kuendelea kufanya kazi kwa umakini mkubwa ili waweze kujikinga wao (nguvu kazi ya Shirika) na familia zao," ilisema taarifa hiyo.

Miongoni mwa hatua ambazo watumishi wa STAMICO na wageni wametakiwa kuzingatia ili kupunguza uwezekano wa maambukizi ya ugonjwa wa corona ni pamoja na kunawa mikono na sabuni, maji tiririka, kutumia vitakasa mikono (sanitizer) na kupima joto kwa kutumia thermal scanner waingiapo ofisini.

Hatua nyingine ni kuandaa mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kujikinga na magonjwa yatokanayo na virusi, ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, kaimu mkurugenzi huyo aliahidi kuendelea kudhibiti maambukizi sehemu ya kazi kwa kuanza zoezi la kusafisha vitasa/milango kwa kutumia dawa (chlorine), kufanya upuliziaji (fumigation) na kuwachukulia hatua wale watakaopuuzia zoezi hili la kujikinga dhidi ya maambukizi.



Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), wakifuatilia kwa umakini mafunzo ya siku moja ya kuwajengea uwezo wa kukabiliana na maambukizi ya Ugonjwa wa COVID 19 na magonjwa mengine ikiwamo yanayoambukiza kwa njia ya virusi) jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Bodaboda kizimbani kwa madai kubaka mwanafunzi

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MKAZI wa Mtaa wa Nyasubi, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Tumaini Julius (28), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama kwa tuhuma ya kubaka mwanafunzi (16) wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Kishimba.

Akisoma shauri hilo la jinai namba 115/2020, Aprili 15 mwaka huu, Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi, Shabani Mateso, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Evodia Kyaruzi, alidai kuwa Tumaini alitenda kosa hilo Aprili 9, mwaka huu katika eneo la Nyasubi.

Mateso alifafanua kuwa Mtuhumiwa alimtorosha mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) na kuishi nae tangu Aprili 3 hadi 9 alipokamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi Kahama.

"Tumaini ambaye ni mwendesha bodaboda, alimshawishi mwanafunzi huyo baada ya kukutana nae nyakati za usiku akiwa anatokea kwa rafiki yake Bukondamoyo. Baada ya kuogopa kurudi nyumbani kwa wazazi wake ambao ni wakali huku akiwa hana nauli, ndipo akamhadaa atampeleka bure kwa wazazi wake, lakini njiani alimwambia waende naye nyumbani kwake Nyasubi na kuanza kuishi nae kama mke na mume," alidai Mateso.

Aliieleza Mahakama hiyo kuwa, Tumaini alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu namba 130 (1)(2)(e) na 131(1) cha kanuni ya sura 16 marejeo ya mwaka 2019.

Tumaini alikana shitaka hilo, hivyo kuahirishwa hadi Aprili 28, mwaka huu na alipelekwa rumande, baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.



# BENZEMA ADOKEZA KUSTAAFIA SOKA LYON

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Karim Benzema, amedokeza anaweza kustaafu soka akiwa Lyon, lakini hana mpango wa kurudi kwenye klabu yake hiyo ya zamani haraka.

Benzema aliondoka Lyon kwenda Madrid mwaka 2009 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 35 na amefunga mabao 241 katika mechi 501 alizocheza kwenye mashindano yote kwa 'Los Blancos' hao.

Iliripotiwa hivi karibuni kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amekubali kuongeza mkataba wake pale Santiago Bernabeu hadi Juni 2022, ingawa hakuna taarifa rasmi iliyothibitishwa.

Benzema alianza kucheza timu ya wakubwa ya Lyon msimu wa 2004-05 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na waliweka historia ya kushinda taji la ligi hiyo miaka saba mfululizo.

Hana shaka kwamba atakuwa sehemu ya kikosi cha Lyon kwa siku za usoni, iwe kama mchezaji au nafasi nyingine yoyote.

"Kurudi Lyon? Mara kwa mara nasema hivyo. Watu wanajua namna gani mahusiano yangu na Lyon yalivyo," alisema kwenye mahojiano na televisheni moja ya Ufafansa.

# Griezmann yupo tayari kupigania namba Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann anaonekana kutokubali kama muda wake wa kucheza pale Barcelona unaweza kufikia mwisho.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kumrudisha nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar na kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.


Imeripotiwa kwamba, Griezmann anaweza kwenda kule San Siro kama sehemu ya mpango wa kumsajili Martinez, lakini Mfaransa huyo hataondoka kirahisi.

Griezmann ameonekana kwamba yupo tayari kupigania nafasi yake pale Barcelona licha ya Neymar na Martinez kutakiwa hapo, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Nyota huyo wa zamani wa Atletico Madrid amefunga mabao 14 katika mechi 37 msimu huu kabla ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29, yupo tayari kupigania namba hata kama Martinez na Neymar watawasili hapo.





# Lukaku hafikirii kurudi tena EPL

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku ametia shaka kama anaweza kurudi kwenye Ligi Kuu ya England, lakini amedokeza majaliwa yake yanaweza kuwa kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, au klabu yake ya zamani ya Anderlecht.

Lukaku amezichezea klabu nne tofauti za Ligi Kuu England kabla ya kuhamia Italia wakati alipoondoka Manchester United kwenda Inter Milan kwa ada ya uhamisho ya uero milioni 73 kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Amefunga mabao 113 katika mechi 252 alizocheza United, Everton na West Brom. Alicheza mechi mbili tu za Ligi Kuu kwa Chelsea.

Lukaku aliulizwa kwenye mahojiano ya maswali na majibu katika mtandao wa kijamii wa Twitter: "Utacheza tena kwenye Ligi Kuu ya England na utarudi Everton?"

Alijibu: "Sidhani, lakini nilifurahia muda wangu pale Everton."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alidokeza uwezekano wa kwenda Marekani au kurudi Ubelgiji, ambako alianzia kucheza soka.

Alipoulizwa kama atafikiria kucheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, alijibu, nafikiria.

## HABARI MICHEZO

# Neuer akasirishwa na Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

MANUEL Neuer amekasirishwa na kuvuja kwa taarifa juu ya makubaliano yake ya mkataba mpya na Bayern Munich.

Golikipa huyo wa kimataifa wa Ujerumani mkataba wake wa sasa na Bayern unamalizika Juni 2021 na kumekuwa na mkanganyiko kuhusu kuongeza muda wa kukaa hapo.

Kipa wa Schalke, Alexander Nubel atawasili hapo msimu ujao, huku taarifa zikisema kwamba, Bayern inajianda kuachana na Neuer.

Iliripotiwa wiki iliyopita kwamba, Neuer alikuwa anataka mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni 20 kwa mwaka, lakini mazungumzo yalivunjika.

Hata hivyo, mazungumzo yake kuhusu mkataba mpya yanaonekana yamevuja kwenye mitandao na hivyo kumkasirisha.

"Nataka kucheza wakati wote nikiwa fiti. Lakini kitu cha muhimu ni uaminifu," alisema Neuer katika mahojiano na gazeti la Bild.

"Ni wazi kwangu kwamba nataka mkataba wa miaka mitano. Nina miaka 34, siwezi kutabiri nitakuwaje nikiwa na miaka 39. Ndio maana kinachotokea kwenye vyombo vya habari hakina maana hata kidogo.

"Nataka mkataba mpya na Bayern ambao utakuwa na masilahi kwangu na kwa klabu ili kila mmoja awe na furaha."





# MADDISON HANA MPANGO NA UNITED

**MANCHESTER,** England

JAMES Maddison amesisitiza "anafuraha sana" pale Leicester City huku akihusishwa na mpango wa kutakiwa Manchester United.

Kiungo huyo mshambuliaji ameripotiwa kuwa kwenye rada za United baada ya kuwa na wakati mzuri zaidi Leicester, ambako aliwasili akitokea Norwich City mwaka 2018.

Lakini sasa akiwa anawaniwa na United, Maddison - ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023 - amesema ana furaha sana pale kwenye Uwanja wa King Power.

"Umekuwa ni wakati wa kuvutia, na nafurahia kila sekunde. Najihisi kuwa nyumbani pale Leicester. Najiona kama sehemu ya maisha ya klabu," alisema akiiambia televisheni ya Leicester.

"Nawapenda watu wa pale, nawapenda mashabiki, tuna kocha mzuri [Brendan Rodgers], hivyo, nina furaha kubwa kuwa pale."

Maddison amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho tatu na kuisaidia Leicester kukaa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England kabla ya kusimamishwa kwa mlipuko wa virusi vya corona.

# *Mancini amfungulia mlango Balotelli Italia*

**ROME,** Italia

KOCHA wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini, amesisitiza milango iko wazi kwa Mario Balotelli kurudi kwenye timu hiyo.

Balotelli hajaichezea nchi yake tangu mchezo wa sare ya 1-1 na Poland Septemba, mwaka 2018 ukiwa ni mchezo wa michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao matano katika mechi 19 alizoichezea klabu ya Brescia kabla ya msimu wa Serie A kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, akiwa amerudi nyumbani baada ya miaka mitatu ya kucheza kule Ufaransa.

Bado, Mancini anajua ubora wa mchezaji huyo ambaye aliwahi kuwa naye pale Inter Milan na baadaye Manchester City kabla ya kuchukua mikoba ya kuinoa Azzurri.

"Kama anafikiria kuhusu soka na anafanya kile anachotakiwa kukifanya, milango ipo wazi kwake yeye na wachezaji wengine ambao hawajawahi kuitwa," amesema Mancini katika mahojiano na Sport Mediaset.

"Mario anatazamwa na kila mtu, ana ubora wake, lakini inategemea na yeye mwenyewe."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARI ANOGEWA NA ARTETA ARSENAL

## ●●● Asema anafurahi kucheza chini ya kocha huyo na anataka kushinda...

**LONDON,** England

NYOYA anayecheza kwa mkopo Arsenal, Pablo Mari, anataka kuendelea kufanya kazi na kocha Mikel Arteta kwa miaka mingi na anamatumaini ya kushinda taji la Ligi Kuu England akiwa na klabu hiyo.

**Beki huyo wa zamani wa Manchester City, Mari alijiunga na Arsenal akitokea Flamengo ya Brazil Januari mwaka huu kwa mkopo wa muda mfupi hadi mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.**

Baada ya kucheza mechi kadhaa na kikosi cha timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alianza kucheza kikosi cha kwanza kwenye ushindi wa 2-0 dhidi ya Portsmouth katika mchezo wa Kombe la FA Machi 2, mwaka huu.

Halafu Mari akacheza kwa dakika zote 90 wakati 'Washikabunduki' hao wakishinda 1-0 dhidi ya West Ham kabla ya Ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Raia huyo wa Hispania amebainisha nia yake ya kutaka kuendelea kubaki hapo kwenye dimba la Emirates, akielezea namna Arteta alivyombadilisha katika uchezaji wake.

"(Arteta) kwa hakika amefanya vizuri hadi sasa. Nina furaha kubwa kufanya naye kazi," alisema Mari akiiambia Sky Sports.

"Amenisaidia kwa udhaifu wangu na nimeimarika na kuwa na nguvu. Natumaini naweza kufanya kazi na yeye kwa miaka mingi.

"Nina vitu vingi vya kujifunza kutoka kwake, lakini soka langu linaweza kuwa zuri zaidi nikiwa Arsenal.

"Natumaini tunaweza kuwa na mwisho mzuri zaidi na nataka mkataba wa kudumu kubaki hapa. Tutaona nini kitatokea kwa sababu kwa sasa tupo kwenye wakati mgumu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona."

Alipoulizwa malengo yake katika soka, Mari alijibu: "Kushinda taji la ligi au kwenda kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa na Arsenal. Pia kwenda timu ya Taifa."

Ligi Kuu ya England ilithibitisha Ijumaa kwamba itaendelea ili kumaliza msimu wa 2019-20 ingawa tarehe ya kurejea haikutajwa, lakini itakuwa mapema Mei, mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### DORTMUND KUMGANDA SANCHO

KLABU ya Borussia Dortmund itampa winga wa timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, euro milioni nne kama ongezeko kweye mshahara wake endapo atakataa kwenda Ligi Kuu ya England. ***(Bild, via Mirror)***

### NEWCASTLE YAMUWANIA VIDAL

NEWCASTLE inaweza kutoa ofa kwa kiungo wa Barcelona na timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ametajwa kwamba anaweza kwenda pale kama kocha wa sasa, Steve Bruce ataondoka na nafasi kupewa Max Allegri. ***(Mundo Deportivo)***

### CORONA KUMSHUSHA MBAPPE

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 21, atashuhudia thamani yake ikishuka kwa euro milioni 35 hadi 40 baada ya mlipuko wa virusi vya corona. ***(AS)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI

KLABU za Arsenal na Everton zinawania kumsajili mshambuliaji wa Celtic, Mfaransa Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22. ***(Le10 Sport)***

### LIVER YAMPOTEZEA WERNER

LIVERPOOL haijafanya mawasliano yoyote na RB Leipzig juu ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 24. ***(General Anzeiger)***

### BARCA KUMUUZA COUTINHO

KLABU ya Barcelona inataka kumuuza winga wake, Philippe Coutinho, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo pale Bayern Munich na ina matumaini kwamba klabu moja ya Ligi Kuu ya England itamsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27. ***(Goal)***

### DISASI AWANIWA ARSENAL

ARSENAL imefanya mawasiliano na Reims juu ya kutaka kumsajili beki wa kati wa Ufaransa, Axel Disasi mwenye umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### SHAQIRI KUSHUSHWA BEI

KLABU ya Liverpool itapunguza bei kwa winga wake, Mswisi Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 28, kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona. ***(Football Insider)***

### BARCA KWA BEKI WA AJAX

BARCELONA inawania kumsajili beki wa kushoto wa Ajax, Nicolas Tagliafico kama mrithi wa Junior Firpo. ***(Goal)***

### LIVER KWA BEKI INTER

KLABU ya Liverpool imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Inter Milan na timu ya Taifa ya Croatia, Marcelo Brozovic mwenye umri wa miaka 27. ***(Libero, via Mirror)***

### BOATENG AITAJA BERLIN

KEVIN Prince Boateng alikuwa na mpango wa kujiunga na Hertha Berlin, lakini amesema kocha, Jurgen Klinsmann alimpuuza. ***(Bild, via Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Katwila atangaza kasi mpya Mtibwa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, ameahidi kurudi kwa kasi ya kutisha na kutoa ushindani wa hali ya juu pindi Ligi Kuu Bara itakaporejea baada ya serikali kuisimamisha kwa kipindi kisichojulikana kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema anatafuta mbinu mbadala za kuifikisha mbali Mtibwa iliyopo nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 33 baada ya kushuka dimbani mara 29.

"Ligi ikianza nitarudi kwa kasi kuhakikisha wachezaji wanabadilisha timu irudishe hadhi Morogoro," alisema Katwila aliyewahi kuichezea timu hiyo kwa mafanikio makubwa.

Katwila aliwataka wachezaji kutumia vizuri muda huu kwa kufuata maelekezo kama vile wakiwa pamoja kambini.

"Wachezaji watumie vizuri muda huu kufuata maelekezo ili waweze kutimiza malengo," alisema.



## New Ston Town yalia na corona

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba, New Ston Town, imesema mlipuko wa virusi ya corona (COVID-19) umeiathiri timu hiyo katika harakati zake za kupanda Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili kocha wa timu hiyo, Mohmmed Suleiman, alisema msimu huu lengo lao kubwa lilikuwa ni kuhakikisha msimu ujao wanacheza Ligi Kuu Zanzibar ndio maana walihakikisha wanafanya vizuri katika michezo yao.

Alisema walitumia gharama kubwa katika usajili wa dirisha dogo kwa kusajili wachezaji wanaoweza kuwapandisha Ligi Kuu, hivyo kusimama kwa ligi hiyo kumewaharibia kwa asilimia kubwa mipango yao kutokana na hofu kwamba msimu ukimalizika wachezaji hao hawatoweza kuendelea kuitumikia timu hiyo kwa mujibu wa mikataba yao.

"Matumaini yetu makubwa tulielekeza katika kupanda daraja na ndio maana tumefanya usajili mzuri na wa gharama ili lengo litimie, lakini hivi virusi vya corona vimeharibu kila kitu," alisema

Hadi ligi hiyo yenye timu 18, inasimama, New Stone Town yenye makazi yake kisiwani Pemba ipo kileleni ikiwa na alama 30 zilizotokana na mechi 13.

# LUSAJO AISHUSHA PRESHA NAMUNGO

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuhusishwa na klabu kadhaa kuelekea dirisha lijalo la usajili, mshambuliaji wa Namungo FC, Reliants Lusajo, amesema kwa sasa mipango yake ni kuwapa nafasi timu yake hiyo kwa kuongeza mkataba wa kukitumikia kikosi hicho kinachotumia Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Lusajo alisema hakuna timu iliyomfuata kutaka kuzungumza naye zaidi ya Namungo ambao walifanya mazungumzo naye kwa ajili kuongeza mkataba.

**Alisema Namungo anawapa kipaumbele kulingana na ofa waliyoweka mezani na kwamba anatarajia kuongeza mkataba wa kuitumikia klabu hiyo watakaporejea kambini.**

"Kuhusu Yanga hizo ni tetesi, hakuna kiongozi aliyekuja kwangu au kupiga simu, zaidi ya viongozi wangu wa Namungo kunieleza nia yao ya kutaka kuongeza mkataba baada ya kumalizika kwa janga hili la corona, mazungumzo bado yanendelea ya kuongeza mkataba mpya," alisema Lusajo.

Alisema endapo Yanga au timu zingine zitamfuata yupo tayari kuondoka kama wataweka mezani dau kubwa kuliko ambalo ameahidiwa na Namungo.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama kutokana na janga la corona, Lusajo amecheka na nyavu mara 11 na kumfanya kushika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji msimu huu akiwa nyuma ya kwa mabao saba dhidi ya kinara, mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagera.

Mabao hayo ya Lusajo yamechangia kuiwezesha Namungo kushika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 50 baada ya mechi 28.

KULALA MWIKO...



Kipa wa Yanga, Metacha Mnata, akifanya mazoezi binafsi Ijumaa iliyopita katika ufukwe wa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam, wakati huu klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID- 19). **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mingange alilia wachezaji kulipwa*

**Na Saada Akida**

WAKATI majaliwa ya kurejea kambini kujiandaa na Ligi Kuu Bara yakiwa hayajulikani kutokana na serikali kutangaza shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ikiwamo michezo kuendelea kusimama, Kocha Mkuu wa Ndanda FC, Abdul Mingange, amewataka viongozi wa timu zote Tanzania kutowatelekeza wachezaji wao hususan katika mishahara.

Kutokana na mlipuko wa kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), Machi 17, mwaka huu serikali ilitangaza kusitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kwa kipindi cha mwezi mmoja ambacho kilimalizika wiki iliyopita Aprili 17, lakini kutokana na hali kuzidi kuwa mbaya ikatangaza zuio hilo kuendelea hadi itakapotangaza vinginevyo.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mingange alisema huu ni muda muafaka kwa viongozi wa klabu kuwathamini wachezaji wao kwa kuzingatia kuwapa mishahara mapema.

Alisema ana fahamu hali ya maisha ya timu za hapa nchini hususan zile za kipato cha chini, jambo ambalo amewataka viongozi kupambana na kuwalipa angalau nusu mshahara ili waweze kuendelea na program za mazoezi yao binafsi.

"Haya mazoezi ya mchezaji mmoja mmoja ni vigumu sana kuwafuatilia hasa kwa kipindi hiki wakiwa nyumbani, kwani mchezaji anahitaji kufanya mazoezi na kula vizuri sasa kutokana na maisha ya wachezaji wetu kutokuwa mazuri kifedha, hivyo viongozi wanapaswa kuwathamini na kuwajali zaidi ya awali wakiwa kambini," alisema Mingange.

Alisema kwa sasa analazimika kuwajenga kisaikolojia nyota wake hao kupambana na kutilia mkazo suala la mazoezi binafsi.

Michezo
Jumatatu Aprili 20, 2020
Nipashe



Mari anogewa na Arteta Arsenal UKURASA 22

EPL? SIRUDI...



Romelu Lukaku akipongezwa na kocha wake Antonio Conte, baada ya kuifungia bao Inter Milan katika moja ya mechi za Serie A msimu huu. Lukaku ambaye alijiunga na timu hiyo akitokea Manchester United ameeleza hafikirii kurudi tena kucheza Ligi Kuu England. **HABARI UK. 20**

# RAGE AKUNWA NA UWEKEZAJI YANGA

## Asema mfumo wa watani wao ni mzuri kuliko wa Simba huku akisifu katiba ya...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Klabu ya Simba kutangulia kuingia katika mabadiliko ya mfumo mpya wa uendeshaji, aliyekuwa Rais wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi hao, Ismail Aden Rage, amesema mfumo watakaokuja nao watani zao Yanga utakuwa mzuri na wenye maslahi zaidi kwa wanachama wao.

**Desemba 3, 2017, Mwenyekiti wa Kamati ya mchakato wa mabadiliko ya Klabu ya Simba, Jaji Mihayo, alimtangaza Mohamed "Mo" Dewji, kuwa mshindi wa zabuni ya uwekezaji baada ya kuweka mezani ofa ya Sh. bilioni 20 akiwa mgombea pekee aliyejitokeza.**

Mchakato ambao umefikia hatua nzuri na mabadiliko ya kiuendeshaji katika klabu hiyo yameanza kuonekana huku Mo Dewji kwa sasa akiwa mwekezaji na mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi wa Simba, ambako atamiliki asilimia 49 za hisa na 51 zikimilikiwa na wanachama wa Simba.

Hata hivyo, wiki iliyopia, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema kwa sasa Sh. bilioni 20 za mwekezaji huyo bado hazijawekwa katika akaunti ya klabu kwa sababu ya kutokamilika kwa mchakato wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji na kufungua kampuni (Simba Sports Club Limited), jambo ambalo wanaamini litakamilika ndani ya mwaka huu.

Alisema kwa sasa fedha hizo zimewekwa katika akaunti maalumu (fixed account) ya Mo kwa makubaliano yaliyofikiwa na bodi ya wakurugenzi na kila mwezi anatoa kiasi cha Sh. milioni 165 ili kusaidia shughuli za kiutawala za klabu hiyo.

Dalili hiyo ya mafanikio ambayo imefikiwa na Simba, imewaibua watani zao Yanga, ambao walishajaribu kufanya hivyo zaidi ya mara tatu wakashindwa, walipoanza mwaka 1994 kupitia kwa marehemu George Mpondela na Tarimba Abbas. Lakini, Rage ameibuka na kueleza kuwa mfumo wa uwekezaji wa Yanga utakuwa mzuri zaidi ya huo wa Simba kwa kuwa wao ni wa 'public' [wananchi] ambao utatoa nafasi kwa wanachama kuweza kuuza hisa zao.

"Kwa mfumo wa Simba wenyewe ni 'private' wanachama hawataweza kuuza hisa, kuna kitu kimejifunga katika mfumo huu wa Simba, ndiyo maana nasema wa Yanga utakuwa mzuri zaidi.

"Ndiyo maana Yanga wanajiita timu ya wananchi, mfumo wao ni kama wa chama changu cha CCM kilivyopitia kabla ya kuitwa CCM," alisema.

Rage alisema hata katiba ya Yanga ni nzuri kuliko yao na mara kadhaa amekuwa akisisitiza si mbaya kuiga mazuri yaliyopo ndani ya katiba hiyo.

Yanga ilitangaza hadi kufikia Mei, mwaka huu itanza rasmi mchakato wa uwekezaji kwa kuingia katika mfumo mpya wa uendeshaji, lakini baada ya mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) vilivyosababisha serikali kuzuia shughuli zote za mikusanyiko, uongozi wa klabu hiyo umeeleza ni kikwazo kwao kuweza kuitisha mkutano wa wanachama ili kupata baraka zao na kufanya marekebisho ya katiba.

## Cavani ni sasa EPL au kamwe?

**LONDON,** England

EDINSON Cavani amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora katika kizazi chake huku...



HABARI UK. 12

## Nyavu Uwanja wa Uhuru na matobo

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Ligi Kuu duniani kote zikiwa bado kwenye karantini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona...

HABARI UK. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >